

CONSTITUTION OF KENYA REVIEW COMMISSION

(CKRC)

VERBATIM REPORT OF

[Redacted]

**CONSTITUENCY PUBLIC HEARINGS, KAJIADO SOUTH
CONSTITUENCY, HELD AT ROMBO CATHOLIC CHURCH HALL**

[Redacted]

[Redacted]

[Redacted]

[Redacted] ON [Redacted]

[Redacted]

[Redacted]

[Redacted]

[Redacted]

[Redacted]

[Redacted]



TUESDAY 9TH JULY 2002

**CONSTITUENCY PUBLIC HEARINGS, KAJIADO SOUTH CONSTITUENCY HELD AT ROMBO
CATHOLIC CHURCH HALL ON 9TH JULY 2002.**

Present:

Com. Bishop Benard Njoroge
Com. Ibrahim Lethome

Secretariat Staff in Attendance:

Joash Aming'a - Programme Officer
Osogo Ambani - Assistant Programme Officer
Alice Thuo - Verbatim Recorder

The meeting was called to order at **9.40 a.m.** with Commissioner Bishop Njoroge in the Chair.

Fr. David Mwangi: Tunaweza kusimama tafadhali.

Baba wetu uliye mbinguni jina lako litukuzwe, ufalme wako ufike, utakalo lifanyike duniani kama mbinguni utupee mkate wetu wa kila siku, utusamehe makosa yetu kama tunavyosamehe na sisi wale wanaotukosea. Usitutie katika ushawishi lakini utuokoe maovuni. Tunakushukuru baba kwa nafasi hii ambayo umetujalia siku hii ya leo tunakuomba baraka zako katika shuguli

ambazo ziko mbele yetu. Tazama tunataka kupeana maoni yetu kuhusu Katiba ya nchi yetu ya Kenya na uturuhusu kwa sababu sisi ni watu wako, sisi ni wananchi wa Kenya, utuongoze ili yale ambayo tutayatoa yawe kwa niaba yetu sisi Wakenya wote na hasa kwa ajili ya ufalme wako hapa katika nchi yetu. Tunakuomba uwezeshe kufika wale ambao wako njiani na tuendeleo kutoa maoni yetu tukiwa pamoja na hatimaye shughuli hizi zikishafika timamu Mungu tuweze kushukuru. Na kuamba ubarikishe haya yote kwani tunaomba na kuamini kwa jina la Kristo aliye Bwana na Mwokozi wetu. Amina.

Com. Bishop Njoroge: Kuna kitu ningetaka kuuliza kwanza Bwana Chief, unafikiri kila mmoja anasikia Kiswahili.

Chief: Wote wanasikia.

Com. Bishop Njoroge: Wote wanasikia. Asante. Jina langu naitwa Bishop Benard Njoroge, mimi ni Commissioner wa Constitutional Review Commission na tuko na mwenzangu ambaye anaitwa Ibrahim Lethome ambaye pia ni Commissioner na ni wakili na ningetaka awasalimie kidogo halafu nitawajulisha wengine.

Com. Lethome: Watu wa Rombo hamjambo?

Audience: Hatujambo.

Com. Bishop Njoroge: Tuna Programme Officer ambaye ndiye atakuwa akijishughulisha na mambo ambayo tunayatenda hapa na ningetaka atujulishe kwa staff wake ili tuwajue na atujulishe jina lake.

Joash Aming'a: Habari zenu? Kwa jina mimi naitwa Joash Aminga, mimi ni Programme Officer, wenzangu ni Alice Thuo ambaye atakuwa akinasa sauti zetu akitumia kinasa sauti na kuna mwenzangu mwengine anaitwa Osogo Ambani, atakuwa akiandika yote yale mlioyasema. Asante.

Com. Bishop Njoroge: Pia katika kazi, kila district kuna mtu ambaye tunaita District Coordinator na kazi yake ni kupanga mambo kama haya na ni mtu wa maana sana na anafanya kazi hiyo na watu wengine ambao pia ni wa maana wanaitwa 3C's na ningetaka Coordinator aje hapa na ajijulishe na atujulishe hawa Committee Members.

David ole Molel, District Coordinator: Wakaazi wa hapa, wageni ambao wamewasili ningependa tu kuwajulisha kwamba jina langu ni David ole Molel, tumekuwa pamoja na nyinyi karibu miezi hizi yote tumekuwa hapa Rombo tukishugulika na hii kazi, na katika kazi hii kama vile Commissioner alivyosema ni kazi ngumu. Ni kazi ngumu lakini ni rahisi ukiwa na watu wako kwa roho yako lakini nashukuru Mungu kwa sababu amenipa wenzangu ambao tumefanya nao siku zote hizi na niko na hao wachache hapa.

Kwanza kabisa ningependa kusema kwamba, mwenyekitu wetu katika Constituency ya Kajiado South tuko naye hapa na yeye ni Bwana Jacob Lesingo na ningemwomba tu asimame ili mumwone. Tunaye hapa Mrs. Amina Abdilahi, yeye ni Member wa Committee yetu, pia tunaye mama Joyce Senewa, Mrs. Senewa tafadhali uonekane. Tunaye Mheshimiwa Mbunge wa Kajiado South, tunatarajia atakuja wakati wowote. Tunao wengine kwa sababu maoni yetu yatachukuliwa kama Constituency na mnajua vile constituency yetu vile iko kubwa tumejigawanya. Tunao wenzetu wawili wanatushugulikia upande wa Namanga na Mile Tisa, kwa sababu leo pia Mile Tisa maoni yanachukuliwa kwa hivyo tunao wawili huko, Mrs. Maruna na Bwana Paul Kaika, wako upande wa Mile Tisa kwa hivyo hawakuweza kuja upande huu.

Tunaye pia Bwana Daniel Somole ambaye hajakuwa hivi hapa na sisi anatushugulikia kwa sababu ya kazi ya kesho pia, kwa sababu kesho tukitoka hapa tutakuwa Loitoktok na pia upande wa Kimanga baada ya kesho. Kwa hivyo hawa kwa kifupi ndio members wetu wa Constituency Committee na ningewaomba tu kwamba tujaribu wote tuweke mawazo yetu pamoja na tupeane maoni yetu vile tu tunavyoongea kila siku tukiwa hapa. Tunasema kwamba hakuna mtu anazuiwa kusema kile alichochacho, kaa ufikirie na uongee na useme.

Kwa hayo machache mimi ningesema kwamba ningewamba Commissioners wetu wanipe tu nafasi kidogo nimshukuru Father wa Rombo Catholic Parish kwa msaada aliyotupatia kutokea mwaka uliyopita mpaka dakika hii tumeweza kuketi hapa. Tumekuwa na yeye, amekuwa nguzo yetu kwa upande wa Rombo, ametusaidia sio tu kwa kutupatia venue, ametusaidia kwa civic education, ametusaidia kuleta wananchi pamoja na ningewamba tu, iwe in record kwamba tunamshukuru sana Father Mwangi. Pia tunawashukuru viongozi, viongozi especially Bwana Senior Chief, Anthony Ole Mepunkuri, amekuwa msaada mkubwa sana kwa upande wa administration, hatuja pata shida yoyote katika area ya Rombo kwa civic education na kwa kila kazi yoyote, tunamshukuru sana. Na kwa hayo machache, ma-Commissioner wangu nawaomba, sasa labda ningemwomba mwenyekiti wetu wa 3C's aje hapa awakaribishe tuanze kazi.

Chairman 3C's: Commissioners, wasaidizi, Bwana Coordinator pamoja na wenzangu wanakamati, wananchi, mtanisamehe kwa kuongea sana ama kufanya haya mpango kwamba naona tumeongea mambo mengi hata sasa..... (inaudible) Nyinyi wananchi tu ndio mimi naomba kama mtu hasikii Kiswahili ama kama husikii lugha, usikae kunyanyaswa kwa sababu hawa sio wa kunyanyasa, hawa ni wa kutusaidia. Tumewaambia mambo mengi mazuri kwamba sasa ndio tunataka ku-rule sio ati kwamba ku-colonise lakini unawaambia kwamba ungependa kuishi namna gani. Leo sio siku ya kusema kuna shida, tuko hivi, natoka mahali fulani, hapana. Go to the point straight away, nende kwenye pendekezo lako, je, unapenda nini iwepo katika Katiba.

Ore ta entoki najoito nai irmaasai, ore oltungani lemeyiolo kiswahili milo ajo iyiolo miyiolo. Tolimu amu ore kulo eti ene tenebo intae.

Na msione kama tuna Njoroge, jina Njoroge hapana Kikuyu, ni Kikuyu tu kwa kujua Kikuyu lakini ni mtu anajua, alikuwa

mwalimu wangu, alikuwa mwalimu wa huyu, alikuwa wa Senior Chief, alikuwa mwalimu wa Manyani, alikuwa mwalimu wa Kilogwa, wale viongozi wenu wote, alikuwa hata mwalimu wa huyu mama. You remember her very well, Amina alikuwa mwanafunzi wako Bwana Njoroge.

Kwa hivyo msione kama kuna ubaguzi, hawa watu ni watu independent na ni watu ambao hawana upande na upande, wewe ndio utakuwa na upande na wewe ndio utakuwa mwongo kama husemi kile kitu unataka. Sema kile kitu unataka iwepo halafu sidhani kama nimewacha mambo mengine, Commissioners, you are welcome na karibu sana. Watu wa Loitok tok hawana mambo mengi, hawana problem, mtasikia vile watasema na tunashukuru.

Ore ta pilimumu entoki enimiyoilo kiswahili tejo mayiolo nilimuni te kisungu amu ejoi itoningu ta.ne enigirakine.

Nafikiri ni hivyo tu, thank you very much.

Com. Bishop Njoroge: Asante sana Bwana Councillor, sasa nimefurahi kwa sababu Amina sikukumbuka. Praise God.

Audience: Amen.

Com. Bishop Njoroge: Kila mahali tunaenda mara tunakuwa na DC, najua DC wa hapa, tunakuwa na DO, tumekuwa upande wa Pokot, Marakwet, Turkana lakini kwa sababu tunawapatia nafasi kutukaribisha kama wasimamizi wa serikali ningetaka kumuita Senior Chief aje atukaribishe na kusema neno moja.

Anthony ole Mepunkori (Senior Chief): Commissioners wetu wa Katiba, wasaidizi wao, kamati ya Katiba katika Constituency ya Kajiado South, wananchi wazee na akina mama *Entasupa pookin, entasupa ake.*

Ningependa tu kuchukuwa nafasi hii kuwashukuru na zaidi kushukuru Commissioners ambao wametoka Nairobi kuja kukutana nasi na kusikiza maoni yetu. Ya pili, nashukuru Father Mwangi ambaye hapa ndio kwake na ameturuhusu kutumia hall hii na ameweza kutusaidia kwa mambo mengi kuhusiana na taratibu ya hii kazi yetu ya siku ya leo. Nashukuru Coordinator Bwana Molel kwa ile kazi anafanya, ile civic education ambayo tumeshafanya katika Rombo, nina imani kwamba leo itakuwa siku njema. Ningependa tu kuwakumbusha kwamba, siku hii mwananchi ni siku yako, leo ni siku yako, Katiba ndio mama ya nchi, ndio mchungaji wetu, Katiba. Sheria hizo ndizo zinachunga maisha ya Wakenya na wewe ni mmoja wao, leo ukikosea, utakuwa umekosea atakeyezaliwa kwa miaka hamsini itakayokuja. Ile katiba ambayo tunatumia sasa ni Katiba ambayo iliandikwa miaka arubaine iliyopita na ssasa hii ambayo tunataka tuandike sasa umeletewa wewe. Ile tuko nayo sasa wananchi hawakuulizwa leo umeulizwa.

Commissioners, nawahakikishia kwamba, area hii ya location ya Rombo ambapo tuko na watu elfu ishirini na saba (27,000)

kwa census ya juzi ndio ina-lead katika Loitok tok District na tuka na makabila nyingi na tuko na areas tofauti za climate. Tuko na areas ambapo ni kavu, tuko na highlands kidogo lakini kwa bahati mbaya wakati huu hali yetu ya mvua ilikuwa ndogo lakini hali ya amani tangu Multi Party wa tisaini na mbili, uchaguzi wa tisaini na saba na unajua sisi tumechanganyikana katika Constituency hii hakuna shida, sisi tumedumisha amani kwa makabila hayo yote na tumedumusha amani hata na Watanzania wenzetu ambapo ni kilometer 2 tu kutoka hapa. Tumedumisha amani na wao na hali yetu ni mzuri. Nawahakikishia kuwa usalama wenu, usalama wa wananchi kwa siku ya leo ni nzuri. Nina imani kwamba Mbunge wetu naye atakuja kuwa pamoja nasi tukija kutoa maoni. Ninaimani kila mtu hata akina mama, vijana, watatoa maoni yao *Ata osiligi nchere ore intae irmaasai olkekun linyi ele emiurere enilimu oltungani entoki nabo amu enilimu nabo kini nepuoyi aiger nepiki embuku ekumbukumbu netapunyo Kenya obulu. Meta aomon intae nchere meesiai hata ninye ena ore eshomoki mpaka enkop pooki ilturkana, imchumari, irkokoyo, longu meta enkop neitu epuo mpaka nepuo lekua oti puani. Entonyok sintae, entolimu ntokitin niyiololo ajo epiki sheria nerat intae tonkolongi napuonu.*

Kwa hivyo basi ningesema ya mwisho kwamba nawahakikishia kwamba tuko salama na siku ya leo Mungu ametujalia ni siku ambayo jua sio kali sana, wananchi wataendelea kuja tu. Unajua nacho kiangazi karibu kimeanza kuingia na kwa hivyo wananchi watachelewa but I am very sure baada ya saa moja hii hall itajaa. Asanteni na karibuni na Mungu awabariki.

Com. Bishop Njoroge: Asante sana Bwana Senior Chief. Sasa nataka kueleza mambo ya Constitutional Review hatujaanza. Bwana Chief amesema na pia Councillor amesema, hii kuja kwetu ni kuchukua maoni yenu, katika Katiba hii hakuna mtu ambaye anamaana isipokuwa mwananchi. Kwa hivyo ukipeana maoni yako, ujue maoni yako ndio inamaana zaidi katika kutengeneza Katiba. Pia sijui kama ni Chief amesema au ni Councillor, hii Katiba itakaa zaidi ya miaka hamsini, kwa hivyo tukitengeneza Katiba hii tuiweke maanani, kwa sababu usiposema sasa lile ambalo liko katika roho yako, utarudi kusema ningejua ningesema haya, lakini utakuwa muda umefanya nini? Umeisha.

Kwa hivyo ninawaomba muwe tayari kusema yale mnayoyaona, hakuna mtu atawazuia. Tumekuwa mahali pengi na tumewaambia hata tukiwa na ma-PC na ma-DC kwamba hakuna mtu atafuatwa kwa ajili ya yale atakayosema. Ie sheria inatusimamia inasema, mwananchi ana uhuru kusema yale anataka kufanya nini? Kusema na hakuna mtu wa serikali anaweza kukufuata kwa sababu ulisema haya. Sawa sawa? Si hapa tumekubaliana? Lakini pia tunasema hivi, usije ukataja jina la mtu kwa njia isiyofaa, sisi tunataka tutengeneze Katiba na Katiba sio mtu. Si ni kweli? Kwa hivyo hatuta taka mtu kutaja majina ya watu kwa njia isiyofaa. Unaweze kutaja useme, tunataka Rais apunguziwe mamlaka, sawa? Hiyo ni sawa, lakini ukienda kusema maneno mabaya juu ya Mbunge au mtu mwingine, hiyo sio Katiba. Si ni kweli? Kwa hivyo ukiwa umekasirika na mtu, mahali pa kutoa hiyo hasira sio hapa, lakini hapa ni mahali pa nini? Pa Katiba.

Bwana Councillor amesema hivi, tunajua shida zetu kama Wakenya, shida za ma-hospitali, watu wamekuwa maskini, wengine hawapeleki watu kwa shule, hizo shida tunayajua, kwa hivyo usituambie shida. Councillor alisema utuambie vile tutafanya ile shida ifanye nini? Ipungue hiyo tu itaenda kwa Katiba na tukifanya hivyo ninajua tutakuwa na mambo ambayo itakuwa ni

muhimu. Mkumbuke, yale mtasema hapa Rombo yatasomwa Kiambu, Lodwar kwa sababu kila report itaenda kila mahali katika nchi gani? Nchi hii, kwa hivyo yale mnasema mjue ni ya maana.

Mtu akija kuongea, tutampatia dakika tano, kama una-memorandum usisome yote, highlight the points. Ikiwa ni memorandum inazungumzia habari ya health, utuambie kama unataka serikali igharimie mambo ya afya. Si ni kweli? Usichukuwe muda mrefu kutuambia mambo mengine, nenda kwa mapendekezo kama vile Councillor alivyosema. Kwa hivyo ukiwa na memorandum, tutakupatia dakika tano, kama huna memorandum tutakupatia dakika tano kuzungumza. Ningetaka pia kusema, hiyo memorandum ukija nayo hata kama hutasoma yote, Nairobi katika ofisi yetu, tuna watu zaidi ya arubaine. Hii memorandum ikifika tu Nairobi, kuna watu wanaingojea, wanaichukuwa na kuweka maneno hayo mahali yanayohitajika. Kwa hivyo msijali hata kama hamsomi yote kuna mahali inangojewa. Sawa sawa?

Pia, kuna kidude hapa karibu na hebu vinuie. Yale maneno utazungumza, yatawekwa hapo, kuna watu huko ofisini mwetu wanaingoja ili wasikize na kuiweka na kuichapa kuenda katika makaratasi. Sawa sawa? Kwa hivyo ukizungumza, ujue pia yale maneno ni maneno ya maana, kwa hivyo usifanye kelele, kwa sababu tukifanya kelele hii kitu itachukuwa nini? Makelele. Na watu watauliza na hawa, walikuwa wapi? Ni Rombo. Kwa hivyo ukisikia mtu akitaja maneno yale hutaki, usijaribu kumzuia, wacha aseme yake na wewe utakuja kusema nini? Yako. Sawa sawa, si hapo tumekubaliana? Kwa hivyo nafikiri mtu akimaliza, ukija kuongea, utakalia pale, utakalia viti hivi. Ukimaliza kusema, utakuja pale ujiandikishe katika register. Ile register ya Kenya ambayo imeonyesha wale wote ambao wamezungumza. Kwa hivyo utakuja hapo, kutoka hapa utakuja wapi? Utakuja hapa.

Sasa nafikiri tutaanza na pia ningetaka kusema hivi, tunaenda na list vile imeandikwa, haturuki kwa sababu mtu ni wa maana isipokuwa labda Mbunge wenu akija tutampatia kukaa kama saa moja halafu tunampatia nafasi kuzungumza. Lakini tukiwa na disabled, tukiwa na mama mjamzito, lazima nitawakubali ili waweze kuzungumza mbele. Tukiwa na wanafunzi wa shule, pia nitawakubali ili wazungumze warudi wapi? Kwa darasa, lakini hawa wengine watafuata vile list vimeenda.

Ningetaka kuita Joseph Nkose. Joseph akija, mtu akimaliza, Commissioner ikiwa ana kitu anataka kujua kutoka kwako atakuuliza swali lakini nyinyi hamuwezi kumuuliza swali. Mnasikia hivyo? Haya sawa. Joseph utasema jina lako, kila mtu lazima akianza anasema jina lake.

Joseph Nkose: Mimi naitwa Joseph Nkose na ningeomba Bwana Commissioner kwanza nawasalimu nyinyi Commissioners, wazee na akina mama. Hamjambo?

Basi tumesema sisi ardhi iliyochukuliwa na Wazungu wakati wa ukoloni, tunataka turudishiwe, tumesema pia Land Control Board hatutaki tena kabisa. Tunataka uuzaji wa masamba ama land control hiyo irudi katika sub location kwa wazee.

Tumesema tunataka Majimbo.

Tumesema pia, mtoto wa kike asiyebahatika kuolewa ni lazima apate urithi kwa baba yake.

Tumesema mali ya asili iliyoko kwetu nchi ya Maasai, tunataka tutawale sisi wenyewe kama wanyama wa pori, minerals zingine kama mito, maji, miti pamoja na madini, quarry, sisi tunataka tutawale wenyewe.

Tumesema sheria number 75 ya Kenya hatutaka sisi tena.

Tumesema pia kesi ya mashamba kuhusu ardhi tunataka irudi kwa wazee wa sub-location waendeshe kesi na wakishindwa iende kotini.

Pia tumesema viongozi wote wachaguliwe na wananchi wenyewe sio mtu moja tu ku-appoint kama ni chief. Hata iwe nomination kwa Council ama nomination kwa Parliament tunataka uongozi huo wote yapitie through wananchi wachaguwe wenyewe. Na sina mengi ni hayo tu kwa upande wangu.

Com. Bishop Njoroge: Haya ngoja kidogo Commissioner ana swali.

Com. Lethome: Bwana Joseph, umependekeza kuwe na Majimbo lakini haukutueleza ni katika kiwango gani. Hayo Majimbo unataka yawe katika kiwango cha wilaya au katika kiwango cha mkoa? La pili, umesema mtoto wa kike ambaye hakuolewa hawezi kumrithi mzazi wake. Ningependa kuuliza kwa sababu sheria inayotutawala hivi sasa imepangia tuangalia usawa baina ya mwanamke na mwanamme. Na je huyo msichana akiolewa kisha awachwe na mumewe kwa sababu inawezekana arudi nyumbani kwao na baba ameshagawa mali tayari. Hauoni kwani tunamdhulumu huyo mtoto wa wakike? Na pia kuna uwezekano, umemgawia shamba kwa sababu hajaolewa kisha baadaye akiolewa je, itabidi anyang'anywe huo urithi ambao alikuwa amerithi? Ningependa ufafanue?

Joseph Nkose: Basi kwa upande wa kurudishwa kwa ardhi yetu ya Maasai, sisi wote tumesema.....

Com. Lethome: Majimbo uwe kwa kiwango gani?

Joseph Nkose: Majimbo iwe katika mkoa.

Com. Lethome: Kila mkoa iwe ni Jimbo?

Joseph Nkose: Uwe ni Jimbo.

Com. Bishop Njoroge: Hilo swali lingine la msichana?

Joseph Nkose: Sasa ya msichana, sisi tunapendelea kwamba, msichana tu asiyebahatika kuolewa ndio tunaweza kukubali awe pamoja na vijana wa boma hilo.

Com. Lethome: Unaona utakuwa unawa-encourage wakose kuolewa ndio wapate urithi na unadhulumu msichana, unamfanya kuwa tofauti na watoto wengine na wote wako sawa?

Joseph Nkose: La, unajua kimila ni lazima mwanamke aolewe.

Com. Lethome: Lazima?

Joseph Nkose: Ni haki mwanamke aolewe.

Com. Lethome: Na asipoolewa?

Joseph Nkose: Atapata share pamoja na wenzake.

Com. Lethome: Kwa hivyo mimi nikiwa msichana wako nitaamua nisiolewe ndio nipata shamba ama unaonaje? Hebu fikiria hilo swali.

Com. Bishop Njoroge: Ningetaka kushukuru Bwana Joseph kwa sababu, mmesikia vile amefanya, points, points na points za maana. Sawa sawa? Tukienda hivyo, tutamaliza na tutakuwa na kitu cha maana, nimeshukuru sana Joseph. Karibu hapa. Tupate Anthony ole Mepunkore, Senior Chief.

Anthony Ole Mepunkori: Ningepeda tu Bwana Commissioner nisome memorandum kwa lugha ya Kiingereza na kutafsiri kwa lugha ya Kiswahili ili iweze kueleweka. My name is Anthony Tumaina Mepunkori and I am the Senior Chief of Rombo Location.

1. Preamble: The Constitution of Kenya needs to identify and to reflect the history of Kenya and the Kenyan people for future reference by the next generation. (Maoni yangu ni kwamba historia ya Kenya na historia ya watu wake iwekwe katika chanzo cha kuandika Katiba ya Kenya mpya).

2. Cultural, ethnic and regional diversity and communal rights:

- I. The Kenya ethnic diversity and cultural norms contribute to a national culture. Mila na desturi ya nchi hii na watu wake inafanya tuwe na mila ya pamoja ya kutuleta pamoja kama Wakenya).
- II. Cultural and ethnic diversity should be protected by the Constitution. (Katiba ambayo itaandikwe ilinde haki ya mila na desturi ya watu wake).

Com. Bishop Njoroge: Can I suggest something Senior Chief? You see when you go to transcribe there will be a problem because, you are speaking the same thing. You either choose to speak in Kiswahili or you choose to speak in English because you see, you are only talking to us, we are the people whom you are supposed to address.

Anthony Ole Mepunkori: The Maasai ethnic diversity and culture should be protected and promoted in the Constitution.

III. The Maasai as a distinct social group should be catered for in the Constitution.

The Maasai language should be identified, recorded, documented for future reference for divinity of future generation.

IV. Only one national language should be maintained as a medium of national communication (Kiswahili).

V. Cultural System of sports, cultural dances be documented for future reference for the future generation Maasai community.

3. Land, natural resources and pastoralism: Land to the Maasai community is the basic of life and foundation of their culture and forms their identity. Proposals:

- i. Section 75 of the Kenyan Constitution should be repealed or altogether reviewed to enable the Maasai community get legal access to their grabbed land through treaties, dubious and unscrupulous means by the State and high placed persons in the community.
 - ii. Land Control Boards to be replaced with Community Land Control Boards comprising of men and women elected among reputable members of the community at the sub-location and the locational levels.
 - iii. All areas of land administration and management should be done by the Maasai themselves.
 - iv. Trust land Act should be done away with and all land put under direct ownership of the Maasai community. The Maasai customary law on land should be enshrined in the Constitution.
 - v. All natural resources be it minerals, wetlands, wildlife and flora and fauna should be put under the administration and management of this community the Maasai.
 - vi. The community should be given priority in all forms of economic benefits and natural resources.
 - vii. Pastoralism as a social and economic livelihood of the Maasai, pastoralism should be recognised in the Constitution.
- Proposals:

A martial plan for pastoralist and pastoralism should be constituted to enable the Maasai community and persons living in arid and semi arid lands to fight / reduce poverty and reach high levels of development.

A Ministry to undertake the martial plan should be formed and constituted.

Industries for processing animal products like hides and skin, beef packaging, milk and slaughterhouse to be developed in all outlets.

The pastoralists be given temporary passports to enable them take their livestock across the international borders in times of weather calamity like droughts and floods.

Livestock diseases control should be constituted and a programme put in place for proper livestock development.

The pastoralists of hardship areas should be given preference in the areas of education, health and employment for the economic benefit.

4. Governance: Proposals:

I propose that Majimbo or Federal Constitution to be put in place. Mikoa like the Rift Valley should be constituted as a Jimbo.

The present system of provincial administration be abolished and local governors to reduce them.

5. Local Government:

Mayors and Council Chairmen should be elected directly by the people.

The two year term for Mayors and Council Chairmen is not adequate, they should be give one, five year term and can be recalled by public interest incase of mismanagement of public resources and misconduct.

There should be a minimum qualification for Councillors, at least form four level of education. Moral ethics should also determine the qualification of a Councillor or an MP.

6. The electoral system and process:

We should have and retain the present representative electoral system.

The winner should guner at least 50% of the total votes cast and if not a repetition should be done.

Candidates should be allowed to switch asess and seek nomination from another party.

We should have seats reserved for interest groups like the disabled, youth and labour organizations.

The demarcation of constituencies and wards are not satisfactory, for Kajiado South Constituency new boundaries should be established to cater for Namanga.

Civic, Parliamentary and Presidential elections should be conducted separately to give voters time to decide on a suitable candidate.

The election date should be fixed by the Constitution, so that the head of state does not use as a political weapon.

Presidential election should be done directly by the people.

7. Basic rights:

The Constitution should guarantee for social, economic and cultural rights.

The Constitution should also guarantee for right of worship.

The death penalty should be abolished and stringent measures taken like life imprisonment for murderers, rapists, robbers with violence and other acts which threaten state security.

Last but not the least, the State should shoulder the responsibility of ensuring that all Kenyans enjoy basic rights like freedom of speech, expression, security, healthcare, water, education, shelter, food, employment and culture. Thank you.

Com. Bishop Njoroge: Thank you very much Senior Chief, you have given us your proposals. Now, you suggest that Namanga.....be removed, are you suggesting that we creat Kajiado South to have more than one constituency or what do you want when this is removed from Kajiado South?

Anthony Ole Mepunkori: I suggest that Loitok tok district should be a boundary of Kajiado South Constituency.

Com. Bishop Njoroge: But you are happy with Kajiado South having one parliamentary Constituency?

Anthony Ole Mepunkori: I have not mentioned it but I think we need two constituencies within Kajiado South.

Com. Bishop Njoroge: Thank you very much, you can record there. I want to recognise the presence of the area DO, as I said before we started wherever we have gone, we have either had PC or DO and now that you have come, I want to welcome you Bwana DO. Do you want to say one thing because we have just started now, I will give you one minute to say something and then you can present later on.

District Officer: Thank you Commissioner Njoroge, Commissioner Lethome and other panelists are gathered at this meeting, wananchi at large, mine is to take this opportunity to welcome you most sincerely to Loitoktok sub district, I did understand that this one is a national exercise, we attach a lot of importance to this exercise, we have gone out of our way to ensure this message has gone to wananchi. First before you got your invitations about the exercise, we had written to the Chiefs, we have publicized in the local Churches and Mosques so wananchi are aware of this meeting. We have told them to come and they have turned up in large numbers so that they can come and give their presentations to the Commissioners because this one is touching on their lives.

Kwa Kiswahili wananchi, nachukua hii fursa kuwakaribisha wageni wetu leo Commissioner Njoroge na Commissioner Lethome, Bwana Coordinator na ma-ofisa wengine walioandamana na hawa kutoka Nairobi kuja kuchukua maoni yenu kama

wananchi wa Loitok tok na nafikiria ijapokuwa sisi tuko na desturi ya kuja mkutano kama wakati umepita ama kuchelewa lakini ninauhakika huo ujumbe umefika kila sehemu ya wilaya ndogo ya Loitoktok. Nimekuwa na mikutano kadha na viongozi, mkutano wa group ranches hata jana tulikuwa pale Mutoko. Kwa hivyo hii ni kitu inahusu maisha yetu na inafaa sisi tupeana maoni yetu hasa mambo ya ardhi, mambo ya elimu kwa Wamaasai. Hiyo ni tatizo kubwa sana lakini mimi mwenyewe wakati nitapewa fursa nitapeana maoni yangu, moja au mawili ama matatu. Asante sana Bwana Commissioner.

Com. Bishop Njoroge: Thank you very much Bwana DO kwa ile kazi umefanya ili tuweze kuwa na watu wengi. Asante sana. Joyce Senewa, Joyce Senewa tafadhali?

Joyce Senewa: Majina yangu ni Joyce Senewa kutoka sehemu hii ya Loitok tok na nitaanza kutoa maoni yangu.

Maoni ya kwanza ni kuhusu uongozi: Katika uongozi wa Bunge, ningeonelea kwamba tungehitaji Rais awe na nafasi ya miaka kumi tu peke yake na asiweze kurudi mara ingine hata kama wananchi watampendekeza lakini iwe mara mbili tu, muda wa miaka kumi. Pia kwa maoni yangu naona kwamba hakuna haja ya kuteuliwa kwa Bunge au Council, madiwani ambao huwa wameteuliwa. Halafu pia katika Bunge, tuwe na robo tatu ya nafasi ya akina mama katika uongozi. Robo tatu iwe ni akina mama na iwe ni lazima wawekwe katika Bunge.

Katika haki za binadamu: Akina mama wawe na haki ya kurithi waume wao hasa wakiwa wako hai. Pia wasichana waweze kurithi kama hajaolewa ama ameenda kwa bwana akafukuzwa akaribu nyumbani aweze kurithi kwa baba yake.

Viwete, waweze kupewa nafasi za kazi sawa na watu wengine na hata katika Bunge au katika uongozi.

Mambo ya elimu: Kuwe katika muongozo wa elimu kuwe na nafasi au somo linalohusu ufugaji au watu wa kuhama hama, (pastorolists). Iweze kuwekwa katika syllabus.

Halafu basi katika hali ya watoto kuingia katika vyuo vikuu, sehemu yetu ya Kajiado iweze kuwa imeangaliwa kama sehemu ya watu wa kuhama hama kama sehemu zingine yaani points zile watoto wanaingia nazo Univesity ziweze kuteremshwa kama sawa na sehemu zingine za ukame. Watoto waweze kuingia wakiwa na C+ au C plain.

Pia katika upande wa afya: Sisi ni watu wa kuhama hama na hivyo kwa maoni yangu ningeomba kungekuwa na ma-hospitali za kuhama hama (mobile hospitals) ili tuweze kufikia wananchi mahali wapo ili tuweze kupunguza vifo katika sehemu ya watu wa kuhama hama. Sina mengi, ni hayo tu.

Com. Bishop Njoroge: Kuna swali tafadhali.

Com. Lethome: Joyce umesema ungependekeza wanawake waweze kurithi waume wao hata wakiwa hai. Mtu anawezaje kurithi akiwa hai?

Joyce Senewa: Katika sheria ya sasa tunajua ya kwamba mwanamme huandika will au urithi wake na kuhifadhi hadi atakapokufa ndio inaweza kutolewa na wakili wake au yule aliyekabidhi. Kwa hivyo tungeona, angeweka haya mambo wazi kama angalihai. Na hapo pia pole ningengeza ya kwamba, katika mila zetu, mama akiolewa na akose watoto, hawezi kurithi ile boma. Kwa hivyo ningependekeza kwamba hata akipata watoto hawa watoto waweze kurithi sawa na wale walio na watoto.

Com. Lethome: Sasa unajua ungesema hivyo badala ya kutumia neno kurithi, unajua ukitumia neno kurithi tayari kifo kimeingia hapo mahali. You cannot talk of inheritance without talking of death, badala ya kusema kurithi tuseme agawanye mali yake akiwa hai.

Joyce Senewa: Haya, tunaweza kutumia hiyo neno.....(inaudible).

Com. Bishop Njoroge: You can come here and register. Can we have Amina Abdilahi? **(Interjection)** Okay, it is alright, Amina okay, tafuta, umepata sawa, karibu.

Amina Abdilahi: Kwa jina naitwa Amina Abdilahi, ningetaka tu kurudia maneno ya Joyce kwa sababu ni kama amezungumza yote. Hasa haki ya wananwake, kuna Wabunge, ningepomba iwe sawa na wanaume, kwa leadership yoyote, lazima akina mama wawe wawili ama watatu, kama uongozi kwa upande wa Chief, DO tupatiwe.

Mambo ya urithi ni haki ya mwanamke asirithiwe na mtu asiyetaka katika boma kama bwana yeke amekufa na kama ana shamba mama arithi kwa sababu ni yeye(Inaudible) bwana yake ndiye alifariki. Kwa mali, azungumze na watoto wake ,yawe ni yeye na watoto wake warithi katika hiyo familia. Urithi iwe sawa kwa msichana na kijana katika boma. Yangu ni hayo tu, sikuwa tayari, ningetayarisha zaidi.

Com. Bishop Njoroge: Lakini Amina umesema mambo muhimu na haya mambo tumesikia kila mahali tumeenda na unafikiria si mambo mengi lakini ni mambo muhimu. Asante sana. Philip Nyakarina. Tafadhali Amina utajiandikisha pale.

Philip Sunde: Kwa majina mimi ni Philip Sunde Nyakarina. Katika profession, mimi ni Secretary wa Rombo Group Ranch. Nimeandika maoni yangu kwa Kiingereza.

Land and property rights: The local community and the individual should have ultimate ownership of land. The government or the Local Authority should not have the power to control the use of land by the owners or occupiers. The nuclear family should

be involved in the transfer and inheritance of land. The DO's should not be Chairmen of Land Control Boards, these boards should be at the village and sub locational levels.

The Executive: There is need for a provincial administration but Chiefs and Assistant Chiefs should be elected by the people.

The Legislature: The MPs should work on the basis of instructions from their constituents and not party. The salary of the MP's should be determined by a Commission and not the MPs themselves. No party should have more than two nominated MP's. All parties should get access to ministerial posts. Ministers and Permanent Secretaries should be given posts according to their qualifications and education levels.

Management and use of natural resources: The community where the resources are found should get 80% of total income and 20% to go to the central government.

The structure of the government: We should adopt a Federal System of Government in which the Executive and the Legislature's authority is split between the Central Government and distinct regional units. The reason being to keep speed development in marginalized regions. This will allow for fair sharing of the resources.

The government should bring back direct compensation for wildlife damage to livestock and food crops. The process of compensation from wildlife killing of a human being should be revived to allow compensation in not more than 6 months time.

Com. Bishop Njoroge: Thank you very much, may be one question. You still want us to retain trust land which are owned by the County Council or you want them abolished?

Philip Sunde: We want them to be abolished and to be under direct management of the community in every region.

Com. Bishop Njoroge: Okay then, the second question. Compensation for death is normally I think, Kshs. 30,000/=, do you want it to be retained at that?

Philip Sunde: Compensation of life is very little compared to the life lost, the Kshs. 30,000/= compensation for a human being is very little compared to the life lost, although the value of a human being is cannot be measured but at least it should not less than Kshs. 1 Million depending on the age.

Com. Bishop Njoroge: Thank you very much Philip. Now can we have Jackson Meliyo?

Jackson Meliyo: Kwa majina naitwa Jackson Meliyo na kuhusu marekebisho ya Katiba ningependelea kwa wa upande wa

utangulizi wa Katiba, kuwe na mwongozo ambao utatuongoza ya miaka ijayo, labda baada ya miaka ishirini ama ishirini na tano, tutahitaji kuelimisha Katiba. Tuwe na mwongozo ambao hautatuletea tatizo kama hili ambalo taifa hili liko nalo. Kwamba, isiwe tunategemea Bunge ndio itatubadilishia Katiba, kwa mfano sasa hivi tunahitaji kwamba baada ya kupeana maoni kama haya hatujui kama ipelekwe Bunge tena yaende yajadiliwe? Kuwe na maoni ambayo pengine itaweza kuwachwa kando, hapo tunawasiwasi kidogo.

Tuwe na muongozo kwamba yale ambayo tutapitisha kama inawezekana yawe yakirudishwa, iwe kwamba wale ma-Commissioners wakienda kukaa, wakae waangalie yale mambo yamepitishwa Kenya mzima na kama uwezekano turudishiwa tujulikana kwamba hayo mambo ndio tukisema na yapitishwe. Na kwa utanguliza wa Katiba tuwe na muda kwamba baada ya miaka ishirini na tano Katiba irudiwa tena upya, iangaliwe kama kuna mambo ambayo yatarekebishwa.

Muundo wa serikali ambao sasa tuko nayo, muundo ubakie vile vile kwamba wananchi wachague kama ni Rais, vile ambavyo iko sasa lakini baada ya kuchagua, serikali mahakama na Bunge ziwe huru kufanya kazi yao. Isiwe na utatanishi ambayo sasa iko, mahakama haifanyi kazi yake, inaingiliwa na serikali kuu. Bunge, kazi yake iwe wazi, isiwe inaingiliwa na serikali kuu. Kwa mfano tusema nchi kama USA, serikali zao ziko na nguvu na uchaguzi unafanywa kama nchi yetu ya Kenya, Rais anachaguliwa moja kwa moja na raia na hiyo serikali inaendelea na kazi vizuri haina shida. Kwa hivyo katika nchi yetu, tukiwa na huu muundo wa sasa na kila upande uwe na uhuru wa kufanya kazi yake nina hakika kwamba kila kitu kitakuwa sawa.

Kwa upande wa Bunge, mimi naonelea wakati wa Bunge saa zingine unakuwa fupi sana, siku tatu katika wiki, wawe wakifanya kazi yao kuanzia Juma-tatu hadi Ijumaa. Na mambo mengine ya Bunge kwa mfano kujiongeza mishahara, wasiwe wao ndio wanajiaongezea mishahara yao, kuwe na Tume ambayo ndio itakuwa ikisimamia kazi yao na kuangalia masilahi yao kama kwa mfano, zile zingine ambazo zinasimamia sehemu zingine katika serikali.

Kuna Wabunge ambao wanachaguliwa na kwa kweli Mbunge anaweza kukaa miaka tano kwa sababu anajua ameshachaguliwa na tikiti ingine ama kitu ambacho kitamsababisha atolewe ni baada ya miaka tano na kura. Kuwe na wakati ambapo tunaweza kumpigia kura ya kutokuwa na imani kama hafanyi kazi, kuwe na percentage fulani kwamba percentage ya 45% ikikubali kwamba huyu Mbunge hafanyikazi kura irdiwe.

Ninapendekeza pia Rais hasiwe Mbunge katika Bunge kwa sababu Rais akiwa Mbunge mara kwa mara haendi Bungeni, unakuta wengine wako Bungeni kazi zingine saa ingine ikiwa iko mahali anasaidiwa haende kwa hivyo tunaomba Rais awe tu Rais, achaguliwe akiwa Rais.

Kwa mabaraza, Madiwani wakichaguliwa iangaliwe pia elimu wao, wawe angalau wamefika form four. Mwenyekiti wa baraza pia, awe amefika form four na akae kwa miaka miwili baada ya miaka misili na nusu hivi uchaguzi ufanywe tena na achaguliwe moja kwa moja na raia si na Councillors wenyewe.

Pia kwa upande wa County Council asilimia ishirini na tano ya yale mapato ambayo yanapatikana katika community irudishwe katika community kwa mfano katika mahospitali kila tafara iwe na hospitali ama dispensary ambayo inasimamiwa na County Council na location ili ile asilimia ya pesa ambazo zinapatikana katika County Council irudi kwa raia moja kwa moja.

Haya katika haki ya ardhi ya kila mwananchi wa Kenya.

Com. Bishop Njoroge: I am going to give you one more minute you have already talked for 6 minutes so, you have one more minute.

Jackson Meliyo: Katika haki ya ardhi Wamaasai wamekuwa katika kipindi cha wakoloni. Kulikuwa na hitilafu kidogo kwa sababu wakati Wazungu walipoingia, ardhi ya Wamaasai ilienda kwa wingi kwa Wazungu na baada ya hao kuondoka hawakurudishiwa. Tunahitaji kwamba Katiba ikibadilishwa ile ardhi ambayo sasa jaijapeanwa kwa mwananchi yoyote, Wamaasai wafikiriwe.

Mambo ya wanyama ya pori iangaliwe ile pesa ambayo mtu anapewa akiuwawa na mnyama ipandishwe kutoka elfu thelathini ifike kama shilingi Milioni mbili na pia mnyama akiharibu shamba la mkulima tuwe na compensation kulingana na shamba na iwekwe percentage kama 10% ya destruction ambayo imefanywa.

Naomba tu kidogo nimaliza kwa sababu ni kweli nimechukua muda.....

Uhusiano ya kimataifa katika Kenya ama katika taifa letu, kuwe na sheria ambayo inasimamia nchi, kwamba tusiwe tunakimbilia tu hizi shirika kama COMESA, PTA na zingine nyingi bila kuona faida ambayo tunapata kwa hizi shirika na zingine zitatuletea hasara. Kama hii COMESA unakuta kwamba wanaingiza bidhaa zao na pengin sisi hatupeleki kwao. Kwa hivyo tuwe na sheria ambayo inasimamia nchi, isiwe tunaingilia tu katika mashirika bila kuwa na uangalifu.

Na katika mahakama, kuwe na mahakama wa kuanzia tarafa, iweze kuenda mpaka mkoa kwa sababu unapata kwamba wakati ambao mtu anapata shida hapa, unakimbia wilayani na pengine huna pesa ya kuenda mpaka wilayani. Unakuta mtu ambaye hajiwezi, inakuwa shida kidogo hapo.

Kwa dini, kuna madini mengi ama madhehebu mengi katika Kenya. Pia ingewekwa sheria ambayo inalinda mwananchi kwa sababu dini zimekuwa kama vitu ambavyo vinatukwaza katika mitaa zetu. Kwamba sheria ya kusimamia hizi madini, kwamba isiwe zinatutaliza katika vijijini. Usiku unakuta kuna dini ambapo watu wanapiga ngoma, asubuhi mpaka jioni, kuwe na sheria kwamba dini kama hiyo ikitatiza mtu, kuwe na sheria ya kupeleka dini hiyo kotini.

Ya mwisho, ningependa katika Katiba hii, iwekwe wazi kwamba wakati wa uchaguzi kuwe na muda fulani ama baada ya uchaguzi wa Rais ama Mbunge, tuwe na mwezi mmoja wa kupokezana katika uongozi na yule kiongozi ambaye ataingia. Kwa sababu katika sheria hii ya Kenya sasa kuna hiyo shida, hata wakati huu, hatujui sasa huyu Rais akichaguliwa labda baada ya December, atakaa kwa siku mbili, au tatu apokezane na huyo mwingine. Kwa hivyo mimi nitamalizia hapo, hayo ndio mahitaji ambayo nilikuwa nayo.

Com. Bishop Njoroge: Thank you very much Jackson, you know I am just excited to hear the views na ni kama mmefikiria haya mambo kwa kirefu sana. Karibu hapa. Pia nataka kuwakumbusha hata kama DO yuko hapa niliwaambia, msiogope kutoa maoni yenu na hivyo tunasema kila mahali hata tukiwa na PC au nani, msiogope kusema kuongea kwa sababu pia DO ni mwananchi na yeye atatoa yake. Si ni kweli? Kwa hivyo na pia ameniambia hivyo yeye mwenyewe, watu wasidhani atachukuwa yale mnasema mko huru. John Olentiti. Na hiyo pia inahusu Mbunge, wakati Mbunge atakuja hapa usiogope kusema yale unayofikiria kuhusu habari ya Wabunge.

John Olentiti: *Ore ta enai na airo enkutuk ormaasai. Aji enkarana John Njiwaine ole Ntiti.*

Translator: Anasema kwamba jina lake ni John Njiwaine Olentiti.

John Olentiti: *Ore enai najo nanu, ore apa tiapa kiata apa sukul epesho.*

Translator: Anasema maoni yake, zamani kulikuwa na elimu ya bure.

John Olentiti: *Nikiata sipitali epesho.*

Translator: Kulikuwa na hospitali ya bure.

John Olentiti: *Nikidol ajo kiyie ina neaku eti te iyiok.*

Translator: Na kwa hivyo maoni yake ni kwamba Katiba ya sasa iruhusu tuwe na elimu ya bure na hospitali ya bure.

John Olentiti: *Ore si ntoyie nemeti kiama ashu etarayie irpayiani neta ore pemiri netum ntokitin tiatua menyee.*

Translator: Anasema kwamba wasichana au wake ambao wamefukuzwa na mabwana zao na wanarudi kwa wazazi wapate nafasi ya urithi.

John Olentiti: *Ore si enepa amu mata nanu iti apa nemedipari iyiok, apa kake enang apa.*

Translator: Wakati wa zamani akiwa kijana, anakumbuka national park ya Tsavo hawakuwa wakifukuzwa lakini sasa wanafukuzwa na kupigwa na ng'ombe wao kuondolewa kwa nguvu.

John Olentiti: *Nearitae iyiok nikiboitare si kuna nguesi.*

Translator: Tunapigwa na wanyama wenyewe wako na sisi hapa, wanachanganya na ng'ombe wetu na mashamba yetu.

John Olentiti: *Na enaikash pe etum si nkishu ina park najing si ngusi meshula.*

Translator: Angeonelea wanyama au ng'ombe wa Wamaasai au wafugaji waweze kupata nafasi ya kufugwa ndani ya national park wakichanganyikana na wanyama wa pori.

John Olentiti: *Na kulie.*

Translator: Ameseama hana mengine ni hayo tu.

Com. Bishop Njoroge: Thank you very much, mwambie tumepata hayo yote na hii shida ya national park tumeipata kwa pastoralists wengine kama Turkana na bila shaka hiyo ni land mark Katiba, shughulikia.

Translator: *Etejo ashe engero enkarna ino ede, nejo ore ina nturiru e park etolumutuo sininye turkana nelimu irpokot ajo enyamalita esiai e park tonkishu enye. Meta ore iltunganak le Katiba eiger.*

Com. Bishop Njoroge: Jacob Lensinko, karibu.

Jacob Lensinko: Yangu mimi, maoni ya kwanza katika ubadilishaji wa Katiba hii, la kwaza kabisa ni uuzaji wa ardhi. Haki ya kuuza iondolewe hivyo nilikuwa nasema, (willing buyer, willing seller itolewe). Iwe kwamba katika mashinani ndio tutakuwa na huo huru, katika Sub Location iende kwa Location halafu iende mpaka kwa division. Pia tungeomba tusiwe na Land Control Board kabisa katika wilaya.

Ingingine ni kwamba provincial administration tusiwe nayo tena, wananchi wawe wenyewe wawe ndio wanachaguwa viongozi, isiwe kwamba mtu kama mimi nikitaka kuwa DO nitaenda kutafuta kazi area kama Loitok tok, sijui shida za Loitoktok sijui za Matinani, isiwe tena hivyo. Mwananchi mwenyewe wa chini awe ndie anajijua zaidi na yule kiongozi mkubwa awe amechaguliwa na watu sio na serikali.

Ingingine ni kwamba, nguvu za Rais naye zipunguzwe kabisa, asiwe na presidential decree ya kusema kwamba President amesema hivi. Asiwe na nguvu hata kidogo ya kusema kwamba kama Rais amesema iwe hivyo, hapana. Iangaliwe katika Bunge, na iwe na nguvu zaidi kuliko Rais. Naye pia kwa upande wa Bunge, Wabunge wasiwe na haki kabisa ya kujiongezea kitu kama mshahara ama ya kujiamulia mambo yao, wawe wanaamua tu mambo ya wananchi lakini wasiwe na nguvu ya kujangaliwa wenyewe. Tuwe na Commission ya kuangalia mambo ya Wabunge nao Wabunge wawe wanaangalia mambo na masilahi ya wananchi.

Ingingine ni kwamba mambo ya natural resources katika sub location mpaka location mpaka wilaya kwa mfano mambo ya KWS, kama Tsavo, Amboselli iwe chini ya wananchi wenyewe, Wamaasai kwa sababu hiyo ardhi ilikuwa yao, wanyama ni wao wanachunga wenyewe, serikali ikae mbali nayo. Iwe ni kwamba sisi wananchi wenyewe wa wilaya hii Kajiado South, kama Amboseli na Tsavo irudi kwa wananchi.

Pia mahali ama wafanyikazi wa mahoteli hata askari wa KWS hata askari wa DO, wawe ni wananchi wa hapa kwa sababu wanajua.

Ingingine nisema Majimbo iwepo kutoka mikoani hadi mashinani.

Ingingine ni mambo ya nomination, mambo ya kuchagua au ku-nominate mbunge ama ku-nominate Councillor kama atakuwa nominated. Mtu kwanza asitafute kura halafu awe rejected na wananchi ndio pia tena awe nominated, mtu akiwa nominated awe mtu ambaye hajawahi kuwa rejected, awe mtu-clean. Kwa sababu mtu hawezi kukataliwa halafu tena awe nominated.

Mambo ingine ni mambo ya haki kwa akina mama. Akina mama wapewe haki kama wazee, wawe na equality kwa upande zote. Asante.

Com. Bishop Njoroge: Thank you very much, nenda ukajiandikishe. Nataka kuchukuwa fursa hii kumkaribisha the Member of Parliament of this area, Honorable Paipai, karibu sana mheshimiwa. Hata kama utazungumza baadaye kutoa maoni yako, sema tu jambo kwa watu wako.

Hon. Paipai: Asante Bwana Njoroge Commissioner rafiki yangu, constituents wangu an Commissioner mwingine na wezee wengine. Hamjambo? Mimi yangu naomba kabisa tusiwe na uoga, tujaribu tuzungumze yale tumefikiria, yale tumejitayarisha kuwaambia Commissioners because this is the only time. Hakuna wakati mwingine tutapata.

Mikiata ae kata nikindim ainoto nikilimunye baa ang naba ana enikiyieu neyieuni nilimu oltungani pookin miure hata nake merai hata enipuku tena aji piimaki onyo.

Tafadhali nasema, wale ambao wamekuja hapa tayari kusema jambo moja au mawili usitoke hapa kama hujazungumza. Jaribu kusema yale yote na umalize kwa sababu hii tu ndio nafasi yako ya kwanza na ya mwisho maishani kutengeneza Constitution yako. Kama hii sasa tulitengenezwa around 1960, 1961 na wale wazee akina Shikuku, na wengine, wao wanabahati wameishi wakakuta ikitengenezwa tena, wewe nina hakika tukitengeneza hii, itachukuwa miaka hamsini, hakuna ninaye muona hapa anaweza kuishi miaka mingine hamsini na awe na fursa labda ya kutengeneza Constitution. So, please ujaribu uwezavyo kumimina yote. Asante sana Commissioners.

Com. Bishop Njoroge: Tunataka Benson Sononka.

Benson Sononka: Yangu nimeandika kwa Kiingereza na nitasoma kwa Kiingereza. Wildlife.

Com. Lethome: Anza kwa majina yako tafadhali.

Benson Sononka: Kwa majina naitwa Benson Sononka.

Com. Bishop Njoroge: Benson, you remember you have 5 minutes so highlight the most important points.

Benson Sononka: Wildlife: Whenever a conflict arises between wildlife and citizens or mwananchi, the interest of citizens should take supremacy. Wildlife to be fenced off to protect citizens and compensation guaranteed for any destruction by wildlife or death to a citizen caused by wildlife. Kshs. 3 Million compensation per citizen for life lost and other properties at the current market value.

Management of natural resources. The community or mwananchi bordering the game park to benefit directly from the proceeds of the wildlife.

Soko huru: A mechanism to be put in place to protect the country from becoming a dumping site for substandard cheap goods thereby destroying local industries and farming.

Natural resources. There should be equitable distribution of national and natural resources. Citizens or communities where natural resources are found should benefit more. Allocation of national and natural resources to be determined through constituencies.

Parliament: The President should not be an MP, the President's constituency is the nation. The President, Vice President, Ministers, Mayors or Council Chairmen to declare their wealth. No pension to all holders of political posts. Members of Parliament to serve for three consecutive terms only. Live coverage of parliamentary proceedings. Parliamentarians to have powers to prolong or dissolve Parliament and not the President. Constituency office to be established. Abolish nomination of MPs.

Land, the group ranches: Subdivision of group ranches, 70% of business plots from the group ranches to go to the members by application. Land Control Boards to be transferred from divisional level to locational level. That is all I had.

Com. Bishop Njoroge: One minute for a question.

Com. Lethome: Umetoa mapendekezo kuwa kusiwe na viti vya Wabunge maalum yaani wanaoteuliwa na Councillors maalum. Sasa kuna hawa watu tunasema special interest groups. How do you take care of these in Parliament and in the Council?

Benson Sononka: We think that those who are elected by the people to represent the whole community.

Com. Bishop Njoroge: But the Act which has mandated the review of the Constitution has specifically told us to take care of the interest groups. So the Act requires that we do something about it. What is your position on that?

Benson Sononka: But I think it the the MPs who are elected by the people and I think those whom you say are special also have a right to vote so the person they are going to vote for will take care of them.

Com. Bishop Njoroge: Thank you very much Benson, nenda pale ujiandikishe. Clementina Kanana. We are very happy to have the third woman, I hope to have very many of them today.

Clementina Lataana: My names are Clementina Lataana Ngoisoi.

1. Gender: Female and male genders to be recognised as equal and complimentary by ensuring that their rights are protected in policy and law and guaranteed equal opportunities with men to play an active role in the development process.

2. Administration: The PC's to declare their wealth. Chiefs and Assistant Chiefs....

Com. Bishop Njoroge: Hebu ngoja kidogo, mnafahamu yale yanayoendelea?

Hon. Paipai: *kijoito iji adolita ajo ore tenepuonunu teneisumi te kisungu tenewueji nemegira ashuku te kimaasai negira iltunganak apuku megira aningu na tenikiendelea te nkata naado neishari iltunganak aiteru airuru tena enaikash tinikiboita pookin kiti atua.kai kingo, keyieuni na te kiswahili elimuni nikipal kisungu ana kai kingo amu eningu kulo tunganak kiswahili meta tenikijo naita kiswahili nikidim ata kiningu pookin. Ka nabo sidai?*

Com. Bishop Njoroge: Haya basi tunyamaze atatumia Kiswahili.

Clementina Lataana: Nimesema wakubwa wa mikoa kabla hawajaingia katika viti watuambie....

Com. Lethome: Anza mwanzo, lile ulianza nalo ni muhimu kwa akina mama hawa.

Clementina Lataana: Nimesema haki ya jinsia, wanaweke wapewe haki sawa na wanaume katika kazi kwa sababu wote wanaweza kuwa wamekuwa na kiwango kimoja cha elimu lakini unakuta kwa sababu moja ni mwanamke, yeye anabaguliwa na yule mwanamume anapewa kazi ya juu kwa sababu huyu mwingine ni mwanamke. Kwa hivyo wote wapewe kazi sawa kulingana na kiwango cha elimu yao.

Ingingine ni uongozi, nimesema wakubwa wa mikoa kabla hawajaingia kwenye viti watutangazie mali yao. Pia nimesema Chifu na wadogo wa Machifu wawe wakichaguliwa na watu katika mlolongo. Kwa sababu unakuta Machifu ni sisi tunawajua na wao ndio wanajua shida zetu. Kwa hivyo sisi tuchague wale tunaowataka na wao wawe wakifanya kazi kwa muda wa miaka mitano na warudishwe katika kazi mara mbili tu kama miaka kuma halafu baada ya miaka kumi warudi nyumbani kabisa tuwachugue wengine.

Ingingine tumesema APs watolewe kabisa warudishwe katika Polisi wa kawaida. Tumesema ichaguliwe shirika ambalo Rais

hatakuwa akitoa sheria kwa Police Force yaani kikundi cha Polisi wawe kabisa wametengena na uongozi wa Rais.

Ingingine ni makanisa, tumesema makanisa yote yapewe uhuru wa kuabudu isipokuwa tu ibada zao zisiwe zinaenda kando ama kinyume na Katiba iliyowekwa. Asanteni.

Com. Bishop Njoroge: Thank you very much for those views. John Waigwa?

John Waigwa: Asante. Kwa jina naitwa John Waigwa, nikiwa mwakilishi wa kikundi cha haki na amani katika Parish ya kanisa ya Katoliki ya Rombo nikielewa ya kwamba Katiba ndio ngao inayongoaza nchi. Tungekata katika hii Katiba, kwanza kabisa ijieleze ni nini na ni ya nani na kwa akina nani na kusudio la hii Katiba na matarajio ya wenyewe. Kwa hivyo ipewe uso na sura ya wenyewe Wanakenya.

Jambo lingine ambalo tuliangalia katika kikundi ni kuhusu uajiri. Hapo tulipendekeza katika Katiba tunaangalia yaani uteuzi wote wa viti vya ngazi ya juu kwa mfano, cabinet na Commissions, Embassies na kadhalika ya ngazi ya kitaifa zisipendekezwe na Rais na vile vile vipitishwe na Wabunge. Vile vile tuwe na Tume ambayo inajitegemea na vile vile hivi viwe na tenure ya office yaani wawe wameajiriwa kabisa bila kuingiliwa.

Katika uajiri, watu wanapojiriwa kazi, itegemea elimu yao na ujuzi wao na vile vile katika malipo yao, walipwe kulingana na kazi yao na katika kazi ambazo ni za kitaifa, ziwe zikionesha vile waajiriwa wameajiriwa kuhusisha nchi yote. Yaani kuonyesha national diversity katika kazi za kitaifa. Iwe kila pembe ya Kenya inawakilishwa katika uajiri huu. Vile vile tuwe na Tume inayojitegemea ya kukadiria mishahara ya wafanyikazi wote wa umma kuanzia wa chini mpaka Rais.

Jambo lingine ambalo tuliangalia ni kuhusu uwezo ama mamlaka ya Rais. Hapa tumesema kwamba iwe kuna uwezekano wa kumwondoa Rais anapovunja ile Katiba ama anapoikosea Katiba. Tuwe na hiyo nafasi ya kumwondoa na vile vile wale wote ambao wamechaguliwa na Rais wahalalishwe na Bunge na vile vile aweze kutangaza mali yake anapoingia katika ofisi hiyo ya urais.

Katiba upande wa elimu, tungependekeza katika Katiba hii tuwe na elimu ya lazima ambayo ni bure kwa watoto wote katika elimu ya msingi. Na vile vile iwe ni jukumu la serikali kuona ya kwamba nafasi za elimu ya ngazi ya juu inaendelezwa kulingana na mapenzi na matarajio ya wananchi. Kwa hivyo isimamie hapo elimu ya juu ya kila aina. Vile vile tukaonelea ya kwamba hii civic education ama mafundisho kuhusu muundo na utekelezaji wa kazi wa serikali ufundishwe katika mashule yote na vile vile katika madarasa ya elimu ya watu wazima na wale social workers wanaohusika vile vile wafundishe wananchi kuhusu civic education kama nchi yao inavyotawaliwa.

Vile vile vyou vikuu vya nchini vya serikali viwe na Chancellors visiwe na Vice Chancellors. Vyoo vikuu vya kitaifa viwe na

Chancellors lakini sio Vice Chancellors. Na ninashukuru, ni hayo tu nilikuwa nimeambiwa kusema kutoka kwa kikundi chetu cha amani ya Rombo Parish.

Com. Bishop Njoroge: Thank you very much for the views. Hebu keti hapo chini?

Com. Lethome: Mwalimu nataka unieleze kidogo, umependekeza kama mambo ya mshahara yafanywe na Tume ambayo iko huru (an independent Commission). Ningependa tu kujua hiyo Tume itachaguliwa na nani? Kwa sababu kama hivi sasa tulivyo, Judiciary, kuna Tume ambayo inaitwa Judicial Service Commission lakini watu wanalalamika kuwa si huru kwa sababu ya uteuzi wake. Wale ambao wako katika hiyo Tume wameteuliwa na mtu mmoja. Sasa hizi Tume ambazo unapendekeza wewe, independent Commission, mteuzi atakuwa ni nani kwa sababu uhuru wake utategemea mwenye kuziteuwa.

John Waigwa: Vile vile lazima kuwe na mwenye kuziteuwa na vile vile mwenye kuzi-vet kama napendekeza. Kama zikipita kwa Bunge na tunawakilishi wetu huko katika kila constituency, kila watapitisha itakuwa ni mapenzi yetu kwa sababu wao wanawakilisha mapenzi yetu katika Bunge. Kwa hivyo ofisi zote za public ziwe zikipitia kwa Wabunge ambao ndio wakilishi wetu moja kwa moja. Kwa hivyo haijalishi ni nani anayependekeza lakini ikipitishwa na Wabunge wetu sisi tunajua hiyo ni maoni yetu. Asante.

Com. Bishop Njoroge: Thank you very much. Steven Ngotiek. Sasa tumefikia watu mia moja, watu mia moja tayari ambao wanataka kuzungumza na tuko tu katika nambari kumi na mbili, kwa hivyo nitakuwa strict na time. Sasa nikikupatia dakika tano utumie dakika tano.

Steven Ngotiek: Commissioners wa Katiba, Coordinator wa district, Mbunge wetu Hon Paipai, Chairman wa Kamati wa ...

Com. Lethome: Stephen, ingia kwenye mapendekezo.

Steven Ngotiek: Haya, sawa sawa. Mimi langu hapa ni machache kabisa kwa sababu mimi ni mtu wa peace and justice lakini tumesha-present sasa nataka kuongezea zangu tatu.

Katika misitu, mimi nataka section 75 itolewe halafu Rais asipate tena kupeana misitu pamoja na Commissioner wa lands.

Pili, sisi tunataka wizara ya pastoralists iwe Ministry of Animal and Husbandry kwa sababu katika Ministry of Agriculture sisi hatupati huduma kamili kwa sababu mahindi iko na board, kahawa ina mahali pao pa kuuza, mambo kama hayo pamoja na agriculture na vingine vingi lakini. Ng'ombe haina pahali pa kuuza kwa hivyo tunataka hio.

La mwisho, tunataka mobile hospitals katika reserve kwa pastoralists kwa kuwa sisi ni watu wa kuhama hama ili tusaidiwe

kuwa na ugonjwa kwa sababu tuna hata misitu tunakaa na wanyama, yangu ni hayo tu.

Com. Bishop Njoroge: Thank you very much Steven, very important points lakini umesama kwa muda mifipi, karibu hapa ujiandikishe. Margaret Keko? She is not in, she is coming? Lesakeu ole Mitiakia? Oh my goodness may be I am the one who pronounced it wrongly. Ningewaomba tusifanye kelele, niliwaambia mkinena hayo maneno yote yatanaswa katika ile machine na itatuletea shida tafadhali, ikiwa ni lazima uzungumze na mtu tafadhali uende pale nje uzungumze ukimaliza unaingia.

Lesareu ole Meitiaki: *Ee nele nanu, nata moruo naleng. Ore tenkarna ai na kaji Lesareu ole Meitiaki.*

Translator: Anasema yeye ni Leareu ole Meitiaki na yeye ni mzee sana na anataka kutoa maoni.

Lesareu ole Meitiaki: *Na iroroki intae pooki.*

Translator: Anawasalimu.

Lesareu ole Meitiaki: *Ore kulo nati ena aji.*

Translator: Wale wote wako katika chumba hiki.

Lesareu ole Meitiaki: *Neti nkeru latoiwo na nkeru e nkeru ainei.*

Translator: Wale watu wako hapa hata sio watoto wake ni watoto wa watoto wake.

Lesareu ole Meitiaki: *Anu ayu enapa kata nagirai aara.*

Translator: Alizaliza mwaka ule wa vita vikuu vya kwanza vya dunia.

Lesareu ole Meitiaki: *Kake mara duo moruo tenkaraki olgilata kake kara moruo .*

Translator: Yeye si mzee kulingana na rika lakini yeye ni mzee.

Lesareu ole Meitiaki: *Oh tata, eini apa lolewa ana ana ake iyiok le nkang pookin.*

Translator: *Kakuya tolimu naba orkinin ashu are. Nintoki alimu lomom kumok.*

Lesareu ole Meitiaki: *Nalimu ajo, alimu ntokitin ane olong etata e siai e tata.*

Translator: Anataka kusema machache tu kuhusiana na kazi ya leo.

Lesareu ole Meitiaki: *Kaomoni ninye nkeru esukul ajo eisoma pesho amu kira masikini nimikiata nkishu.*

Translator: Anasema kwamba elimu ya watoto iwe bure kwa sababu umaskini umezidi.

Lesareu ole Meitiaki: *Nairuko, neiruko irmaasai arik enkeru sukul peisuma kake kira masikini naomon sheria pedol*

ajo eshomo nkera ang sukul na egira aisum pesho.

Translator: Kwa sababu sasa jamii ya Wamaasai wamekubali kupeleka watoto wote shuleni lakini umaskini umekuwa mwingi kwa hivyo anaomba sheria ione kwamba watoto wamejengewa shule na wapeleke watoto bure.

Lesareu ole Meitiaki: *Neisumakaki nkera pesho pemebatata enkop.*

Translator: Mnisomeshee watoto ili nchi hii isianguke.

Kakuya nyaki tolimu enkae.

Lesareu ole Meitiaki: *Ata enkae toki, ore ilaiguenak na keaku ajo iltunganak logelu amu ore keyauni oltungani lemeitu eisuma nemeyiolo esiai na ikiyieu neingor ena Katiba ajo iltunganak ogelu ilaiguenak.*

Translator: Anasema kwamba katika utawala wa mikoa na zaidi machifu, siku hizi wanachaguliwa na serikali na mwananchi hajui, analetewa mtu ambaye hajui kazi, hajasoma, hashughuliki na kazi ya wananchi. Kwa hivyo angependa Katiba ione kwamba wananchi wanachagua viongozi wao Machifu.

Lesareu ole Meitiaki: *Ayieu nemokini anyoru olaiguenani neaku iltunganak ogelu.*

Translator: Angepende kwamba watu wapende Chifu na wamchague wao wenyewe.

Kakuya nyaki tolimu enkae. Na tinidipa duo niyo ashe.

Lesareu ole Meitiaki: *Aidipa ashe.*

Translator: Asante, amesema amemaliza.

Com. Bishop Njoroge: Stanley ole Kingi, Stanley yuko?

Stanley ole Lesoi: Mimi kwa jina ni Stanley ole Kingi Lesoi, Chairman wa Rombo Sub-Location katika area hii.

1. Marekebisho ya Katiba, tunataka muundo wa serikali ya Majimbo. Nchi yetu ya Wamaasai tuna uwezo wa kujisimamia kiuchumu, tuna uwezo wa mali ya kuendeleza nchi yetu.
2. Tunataka nchi yetu iwe na title moja na mamlaka ya Council iondolewe na kamati ichaguliwe watakaosimamia plots na Councillors wapeane plots pamoja.
3. Wanyama ni mali yetu na wanakaa kwetu basi serikali na sisi tugawe kati kati maziwa wanaokamua na mnyama akiua mtu serikali ilipe milioni moja na nusu badala ya elfu thelathini wanaotulipa.
4. Mila: Mila yetu Wamaasai ikae vile vile ilivyo na wale wanaiga mila yetu kama mavazi walipishwe.

5. Elimu: Tunataka watoto wetu wasomeshe bure hadi chuo kikuu na nambari grade ile ambayo ni ya juu iteremshwe ili tupate kusoma.
6. Machifu wachaguliwe kwa kura na wananchi la location yake kama Wabunge na Councillors.
7. Mwanamke ambaye hajaolewa na hana tumaini wa kuolewa sharti apewe urithi na baba yake kama watoto wengine.
8. Mkataba waliowekewa Wamaasai na wakoloni, nchi yetu isiingiliwe na makabila mengine idumishwe kuendelea hivyo.
9. Mbunge asiye hudumia wananchi waliomchagua abadilishwe kabla kufika wakati wake wa uchaguzi na kuchaguliwa mwengine.
10. Kamati inayohusika kununua au kuuza mashamba ofisini waondolewe ibaki kwa wazee waliochaguliwa katika location hiyo kwa sababu hao wanajua sababu zaidi kuliko ile kamati wa ofisi.
11. Tunataka Wamaasai wawe ndani ya marekebisho ya Katiba na wahakikishe mabarua zetu zimefika na zimehifadhiwa kikamilifu.
12. Waajiri wa watumishi wa serikali iwe ikifika kwa kiwango ya tarafa ili wananchi wawe wakihudumiwa wakiwa karibu. Ni hayo tu.

Com. Bishop Njoroge: Asante, kuna swali moja hapa.

Com. Lethome: Swali moja tu, ulisema kuwa mila ya Wamaasai ihifadhiwe na mtu mwingine ambaye ataiga mila yao aweze kulipa faini. Sasa unaonaje kwa mfano, hivi sama kama Wakenya tunatafuta nguo ya kitaifa, mavazi ya kitaifa na vile vile naona inaelekea kwa Wamaasai, sasa unaonaje kama mavazi ya Kimaasai itafanywa kuwa ndio nguo ya kitaifa? Mila ya Kimaasai ifanywe ndio mila ya kitaifa, unaonaje?

Stanley ole Lesoi: Naona watu wengine wanakuja kuvaa kama Maasai wanaenda kufanya biashara nayo, kwa hivyo iwe mimi ndio naenda kufanya biashara nayo kwa sababu mimi ndio Maasai.

Com. Bishop Njoroge: Ningetaka pia kuwajulisha, kuna watu wawili wamesema wanataka kujua kama maoni yao yatahifadhiwa. Nataka kuwahakikishia katika ile sheria ambayo imeunda Commission hii imesema kwamba tukimaliza constituency hii ya Kajiado South, tutaandika report inayosema completed report of Kajiado South na pia sheria inasema, kuna

wakati tutaleta report hiyo hapa kwa siku sitini mwangalie kama yale mliyosema kweli yako katika report. Kwa hivyo hakuna mahali itapotea mzee, sawa?

Com. Lethome: Nina swali lingine kidogo mzee, umesema mwanamke ambaye amepoteza matumaini ya kuolewa huyo arithi shamba la baba yake. Tungependa kujua ni umri gani ambao mwanamke anafika na sasa tutasema amepoteza matumaini. Na je, baba akifa kabla ya huyo msichana kufikisha hata umri wa kuolewa, utaamua kuwa huyo ataolewa kwa hivyo asirithi na huyu hataolewa kwa hivyo arithi? Utawezaje kuamua, si unaona tutaumiza msichana?

Stanley ole Lesoi: Hiyo sasa itategemea yule baba ya msichana huyo anaona mtoto wake kweli hataweza kuolewa...

Com. Lethome: Na dalili gani itakuonyesha huyu msichana hataolewa?

Stanley ole Lesoi: Mzee anaweza kukaa kwa muda mrefu bila mtoto wake kupata bwana.

Com. Bishop Njoroge: Okay, asante sana mzee. Moses ole Nitwaasi.

Moses ole Nitwaasi: Basi nami kwa jina naitwa Moses ole Nitwaasi na mimi pia nimeshukuru kwa kupata hii nafasi ya kuweza kutoa maoni yangu. Mimi kwenye maoni, haya maoni nimetoa kulingana na jinsi imeandikwa kwa kitabu hiki kwa hivyo mini nimetoa maswali kupitia kwa hii kitabu. Nikasema kwamba yangu itakuwa ni memorandum ambayo mini nitapeana kwa sababu nimewacha nakala yangu lakini hii nitapeana iende ikachambuliwe vile niliandika na iweze kujulikana ni nini. Kwa hivyo yangu ni hayo tu, muweze kusoma maanake nikisoma nusu haitamalizika ni heri nitoe kama memorandum.

Com. Bishop Njoroge: Sawa, njoo hapa itawekwa kwenye file. Saroni ole Makuna.

Saroni ole Makuna: Ninaomba mtu wa ku-translate.

Saroni ole Makuna: *Ore ta nanu naji Saruni ole Makuna.*

Translator: Jina lake ni Saroni ole Makuna.

Saroni ole Makuna: *Na ore point ai e kwanza na ke enasiai naihusu majimbo.*

Translator: Jambo lake la kwanza ni kwamba angependa utawala uingie kwa Majimbo.

Saroni ole Makuna: *Ore olungani apa olotuiwuni apa enatoiwoki neita ine wueji eshuko alo.*

Translator: Anasema kwamba yule ambaye hakuzaliwa katika Jimbo hilo arudi mahali alitoka.

Saroni ole Makuna: *Ore enkae point eare.na ena siai naihusu irbungei.*

Translator: Anasema jambo ambalo atazungumzia ni mambo ya Wabunge.

Saroni ole Makuna: *Menarikino peaku ninche idungoki ate mpisai nara mushahara.*

Translator: Wasiwe ndio wanazungumzia mambo ya mishahara.

Saroni ole Makuna: *Pe meaku erem ena siai raia.*

Translator: Ningependa kwamba raia wazungumze mambo ya Wabunge wao.

Saroni ole Makuna: *Ore enkae euni, ena siai naihusu mpaka olchambai eti nai ana location ang neaku nabo title olchamba lena kop.*

Translator: Anasema kwamba anataka title iwe moja kwa wale katika location.

Saroni ole Makuna: *Pepiki engolon pemeitoki oltungani ata engolon namirie olchamba lenye.*

Translator: Ili mambo ya uuzaji wa mashamba isiendele.

Saroni ole Makuna: *Enkisuma.*

Translator: Masomo.

Saroni ole Makuna: *Ayieu enkisuma neaku ene pesho ana apa nikipira aitayu kodi ontokitin pookin nikilakita.*

Translator: Angependa masomo ya watoto iwe ya bure kwa sababu ya ile kodi ambayo inatolewa na wananchi.

Saroni ole Makuna: *Enkae eimiet.*

Translator: Ya tano,

Saroni ole Makuna: *Sipitali kiyieu neaku ene pesho.*

Translator: Hospitali na matibabu yawe ya bure.

Saroni ole Makuna: *Esiai onkishu.*

Translator: Kazi ya ufugaji.

Saroni ole Makuna: *Kiyieu nemokini apik esiai onkishu ana ngiri budget ana enoshi serikali budget kahawa ormajanini osukarini. Ikiyieu nepuonu si ngiri ata budget.*

Translator: Anasema kwamba ufugaji nao uangaliwe katika Katiba ili katika makadirio ya pesa ya serikali kazi ya ufugaji tupatiwe sehemu ya pesa.

Saroni ole Makuna: *Esi ai olaiguenak.*

Translator: Kazi ya utawala upande wa Machifu.

Saroni ole Makuna: *Kiyieu nai kore sirikali ogelaki iyiok laiguenak arashu bungei peaku ore ina gelare na pe raia nagelaki ate lelo tunganak amu raia oshi oramat laiguenak neme serikali.*

Translator: Anasema kwamba kuchaguliwa kwa Chifu au utawala katika location iwe ni wananchi wenyewe ndio wanamchaguwa kwa sababu yeye mwenyewe ndiye atachunga masilahi yao, sio Mbunge au serikali iwachagulie wananchi mtu wao.

Saroni ole Makuna: *Councilani.*

Translator: Anaongea kuhusu Councillors au Madiwani.

Saroni ole Makuna: *Mikiyieu irkansolani are ota engolon naishoyo plotini openy moopeny.kiyieu neaku ore ploti na abori ilopenye eti wazee irpayiani le baraza.*

Translator: Anasema kwamba Diwani asiwe na nguvu ya kupeana ardhi katika area hiyo ambapo amechaguliwa, kama ploti iki chine wa uangalizi ya wazee.

Saroni ole Makuna: *Entito.*

Translator: Msichana.

Saroni ole Makuna: *Nata eshal emaoi emaima arashu modooni nalazima peishori uridhi ninye ana olayioni, kake ore eneti engolon nemeishori.*

Translator: Anasema kwamba msichana awe kwamba hana macho ama hajiwezi apate urithi wa wazazi wake lakini yule ambaye anajiweza na ananafasi ya kuolewa asipate urithi.

Saroni ole Makuna: *Ore tena nabo si nata, naomon oleng iltunganak le Katiba apik engolon kuna lomom nikitejo peebaya enayieni.*

Translator: Anasema kwamba ya mwisho angependa Commission ya Katiba ione kwamba maoni haya yanafika pahali yanatakikana yafike.

Saroni ole Makuna: *Ajo ashe oleng.*

Translator: Anasema asante.

Com. Lethome: Hold on, umesema katika hii Majimbo mtu ambaye hajazaliwa katika Jimbo fulani atoke katika hilo Jimbo,

hauoni kama hii italeta ukabila, Kenya itagawanyika katika makabila? Kwa mfano kama mimi ni Mjalu na nimenunua ardhi hapa kwa Wamaasai naishi hapa kwa Wamaasai, uniambie niende kwetu, na mimi si nitaenda kufukuza Wamaasai wale wako huko Nyanza warudi hapa, ama unaonaje?

Saroni ole Makuna: *Ajo ina.*

Com. Bishop Njoroge: Ngoja niongeze hivi, katika sheria inayotutawala ambayo tuko nayo katika marekebisho inasema kila kitu tunayofanya lazima iweze kufanya unity ya taifa ikae pamoja, hakuna sheria ambayo itavunja taifa ambayo itapata njia ya kuingia. Utasemaje kwa hiyo?

Saroni ole Makuna: *Najo ina eini apa ntokitin neti ene wueji eingua kore pi nyangua olchamba ningua.*

Translator: Anasisitiza kusema yule mtu ambaye amenunua shamba katika Jimbo arudi pahali alitoka na yule ambaye amezaliwa katika Jimbo arudi mahali alitoka.

Com. Bishop Njoroge: Thank you, ni maoni yako hayo. Asante sana mzee kwa maoni hayo, njoo hapa. Kila maoni ni muhimu, mnasikia? Na lazima itafika mahali inahitajika kufika. Marki ole Manyapela.

Marki ole Mayapela: *Airo ta tenkut ang.*

Translator: Anasema kwamba ataongea na lugha ya Kimaasai.

Marki ole Mayapela: *Ore na kulo arikok le Katiba orpayiani pookin otaboutwa tenatumo nake airoroki.*

Translator: Anawasalimu tena.

Com. Lethome: Jina?

Marki ole Mayapela: Jina langu ni Marki ole Mayapela.

Translator: *Tinyikaki ine wueji peno.*

Marki ole Mayapela: *Kijoito na kiyieu irmajimbo, na ore entoki nikidol ajo sidai teyiok kidol ajo ore olaiguenani tenangas aku esiai olaiguenak orbungei napekigelaki ate.*

Translator: Anasema kwamba kwa upande wa utawala wananchi wenyewe wamchague Chifu au mtawala wa location na wamchague kama vile wanamchagua Mbunge.

Marki ole Mayapela: *Ore te nanu kajo pebik ake oltungani loshi arin nabiki te serikali wo aolaiguenani orbungei neitoki.*

(Interjection)

Com. Bishop Njoroge: Ngoja mzee, tunasikia watu wanapiga makelele na sasa nitawaambie watoke nje wakazungumze nje. Kikao cha Katiba ni kikao cha muhimu sana na sheria hairuhusu mtu kufanya kelele wakati mtu mwingine anatoa maoni yake. Ikiwa ni lazima mzungumze, usizungumze kwa sauti na ukitaka kuzungumza kwa sauti, mtoke pale nje mzungumze, mkimaliza mnarudi ndani ya nyumba. Tafadhalini tuheshimu yule anayezungumza.

Translator: *Eomonitoi intae tafadhali entigirata petumoki atolimu ena siai amu esiai etipat oleng.*

Marki ole Mayapela: *Neku ajo na ore na lelo pekigelu nebik ake loshi arin lobik te serikali peenalaikino iltungani atoriko iyiok nikipu amu mikipuo si pemeeta olaiguenani loitining entoki na kiyieu ake nebik lelo arin nenangari lopa nikinanga ta kitemena.*

Translator: Anasema kwamba watawala wawe wanachaguliwa kama wanasiasa, akae miaka mitano kama mwanasiasa, akionekana kwamba kazi yake haiendi vilivyo, wanamtupa, wanamchaguaa mwingine.

Marki ole Mayapela: *Ore ene wueji enkisuma onkera nikijo kiyieu neisomakini iyiok nkera serikali.*

Translator: Anasema kwamba serikali ichukue jukumu la kusomesha watoto bure.

Marki ole Mayapela: *Amu kigira tata aisum inkera kake mikiata na engolon netagolo sukul naleng meta etaruoyie enkop.*

Translator: Anasema kwamba gharama ya elimu imekuwa juu sana na kwa hivyo mtu wa kawaida anashindwa kupeleka watoto shule kwa sababu ya gharama, kwa hivyo angeomba kuwa Katiba isisitize elimu ya bure.

Marki ole Mayapela: *Ore ene wueji onguesin najo kitudumuo apa ilchamba lang nikipu netijinga nguesi nenyaka aitinyik emupak meewuo agiru olopa tinga le mishiaki nikiyieu nai neshuki ena paka meshomo abaiki ilopa tinga le mishiaki amu ore ta irnkajaoni ana naiishorua enkai eiputa ilchambai lang near iltunganak kiyieu nai na nikijo, ore si ninye ana empaka amu keyiolo ake kanjaoni dama o kewarie na ina pearita iyiok. Ore peaku olameyu nemeitokini aar iyiok empaka nikinya siiyiok nikipuo ashulare nena nguesi amu mekure kidim teneari iyiok amu inkishu ang na tenkaraki kiramati iyiok enkop ang.*

Translator: Anasema kwamba kwa upande wa National Park ya Tsavo ambayo group ranch hii iko karibu, wanyama wa pori kama ndovu wameingia katika group ranch kwa wingi wanauwa wanyama, wanauwa watu, wanaharibu mashamba, wanaharibu mazingara, angesema kwamba sisi wafugaji tupatiwe nafasi ya kufuga ndani ya park wakati hali inakuwa ngumu ili tundelee kuchanganyana na wanyama hao wa pori, katika national park.

Marki ole Mayapela: *Ore na ana kiti na enkop ang ormaasai, kidungo apa kimbuta ai kidungo dungoki ilchbani meta ore oltungani olotu mekure eta eneijing.*

Translator: Amesema kwamba hakuna pahali, hakuna ardhi ambayo inakaa bure katika nchi hii ya Wamaasai, nchi yote inatumika na kwa hivyo haingekuwa jambo la busara watu wengine wasafiri kuja kuingia hapa kwa sababu tumeshajaa na ardhi yote inatumika.

Marki ole Mayapela: *Kake mikimir ake oltungani oinyangua apa olchamba tene tene noto te bahati mikijo si entarai amu iyiok otimirakitia.*

Translator: Lakini yule aliyenunua, hatusema kwamba tumfukuze, akae pamoja nasi na tuendelee pamoja na yeye.

Marki ole Mayapela: *Neaku aitabaiki ta ine, ashe.*

Translator: Anafikisha hapo na anasema asante.

Com. Bishop Njoroge: Asante sana mzee kwa maoni hayo mazuri, karibu ujiandikishe. Louis Mbalusi. Karibu.

Louis ole Mbalusi: Kwa jina ni Louis ole Mbalusi. Maoni yangu ya kwanza kuhusu Katiba ni sisi tumiliki nchi yetu, hii ardhi yetu hapa.

Translator: *Iroro kimaasai.*

Louis ole Mbalusi: *Ore entoki najoito tena kata iji na ore entoki ena Katiba peyieu elimu esipata tenkop ang.*

Translator: Anasema kwamba maoni yake ni kwamba anatoa maoni yake ya dhati kuhusiana na nchi yao.

Louis ole Mbalusi: *Na ore esipata edukuya nalimu na ena rasmili niyo nkariak.*

Translator: Anasema kwamba wapewe haki zao kulinda rasilmali kama ardhi.

Louis ole Mbalusi: *Amu kore apa olari le ntomoni naudo opishana eishorua apa ina kata aisho iltungani parmit nikincho enkare openy nemeesipata.*

Translator: Alikuwa anasema kwamba kuna wakati kama mwaka wa sabini na tano watu walikuwa wanapatiwa permit ya kumiliki maji mwenyewe katika mto na angesema Katiba iangalie hao watu wasiwe wanapatiwa permit watumie maji wenyewe, watumie kama community au jamii.

Louis ole Mbalusi: *Ore si enkae ne ena siai ongues.*

Translator: Jambo lingine ni rasilmali ya wanyama pori.

Louis ole Mbalusi: *Ore kulo shangit etuo apa neifuruga kiti iyiok enkop ang near iyiok, near inkishu kake melakitae nadoi ana vile medolitaie ajo ekirai aiumisawa wananchi.*

Translator: Anasema kwamba rasilmali ya wanyama wa pori kama ndovu wameingilia jamii ya huku wakauwa wanyama

wao, wakauwa wao wenyewe, wakaharibu mazingara na hawalipwi vilivyo. Angeomba Katiba iangalie kwamba watalipwa ridhaa.

Louis ole Mbalusi: *Ore si ankae na, ore maoni nadolita ore ebaiki nineteen eighty seven nakata iyiok kintetutwa irmaasai ajingaki esiai enturore.*

Translator: Anaeleza kwamba Wamaasai wameanza kujua na kutumia ardhi kwa upande wa kilimo.

Louis ole Mbalusi: 1987.

Translator: Kuanzia mwaka wa themanini na saba.

Louis ole Mbalusi: *Ore ebaiki ina kata mpaka tena kata inji eta kiturisho melio faida nikitum amu etaruoyie uchumi enkop.*

Translator: Wakati huo mpaka sasa tunalima bure, tunatoa vitu vyetu, mimea yetu tunavuna lakini soko imeharibika kwa sababu ya soko huru.

Louis ole Mbalusi: *Kore kulingana na ina soko huru, egira aiumisa sana sana iltunganak oti kulo wananchi tata iji kutiti tene wueji la koon oshi eitegemea ena alo puani meta hasara ake kigira aingoru.*

Translator: Kwa hivyo mwananchi wa chini anaendelea kuwa maskini kwa sababu akitoa mali yake kidogo kwa shamba akipeleka soko la Mombasa, hapati kitu kwa hivyo umaskini umeendelea kwa mwananchi.

Louis ole Mbalusi: *Meta teneidim nai neidimayu peingorakini na sokoni tenewueji peidimayu peepiki esipa peingorakini sokoni nikiya kuna mali oshi nikintau nikijo nai ina peingorakini iyiok engae toki amu ore ake enena eta sokoni ne uhuru.*

Translator: Kwa hivyo angesema kwamba mavuna yao ya mashamba Katiba itafute soko ya kutosha ili wafaidike.

Com. Bishop Njoroge: Can you tell us the last point?

Translator: *Olakuya kitiakaki pilimu ena bayie.*

Louis ole Mbalusi: *Ore enabayieu na ore ntoyie eyieu neingora ena serikali peaku ake ninche eaku ofisa tesiai e serikali entito olayioni amu gharama nabo ake engar pookin eisuma.*

Translator: Anasema yake ya mwisho, vijana wake kwa wanaume wawe sawa mbele ya sheria ya nchi, wawe sawa kwa kila kitu, kwa sababu hata kuwalea katika elimu na kuwalea nyumbani wanatumia gharama moja kwa hivyo wapate haki zao.

Louis ole Mbalusi: *Ashe oleng.*

Translator: Anasema asante.

Com. Bishop Njoroge: Asante kwa neno hilo, soko itafutwe kwa mazao. It is very important. Asante kwa maoni hayo. Kayi ole Kingi.

Translator: *Interu tenkarna ino tolimu enkarna ino nintoki alimu duat inono are uni pe itumoki airo.*

Kayi ole Kingi: *Kaji ta nanu Kayi ole Kingi.*

Translator: Kayi ole Kingi

Kayi ole Kingi: *Na esiai onguesi aimaki tene.*

Translator: Yeye akikaa hapo angependa kutaja mambo ya wanyama wa pori.

Kayi ole Kingi: *Esiai ekulo kanjaoni.*

Translator: Anaongea juu ya hawa ndovu.

Kayi ole Kingi: *Meta kiremisho meta peno nikitum entoki.*

Translator: Wakilima ni kazi ya bure, wakishalima ndovu wanaharibu mimea kabisa.

Kayi ole Kingi: *Etara apa irkanjaoni ilchambi apa eishutua eremore.*

Translator: Ndovu wamemaliza mimea na kuharibu faida ambayo ingepatikana katika mashamba hata na kuua watu.

Kayi ole Kingi: *Nikiyieu nikiomon ta ajo kiyieu neingorari ilkanjaoni pe eyiolou eneikuni.*

Translator: Kwa hivyo ningeomba kusema kwamba katika Katiba hii wangaliwe wanyama wa pori, watu wawe wanalipwa ridhaa na serikali iangalie mambo ya wanyama wa pori kwa upande wa jamii ya Wamaasai.

Kayi ole Kingi: *Neaku ina ta maoni ai nanu.*

Translator: Yeye anasema hiyo moja na anashukuru.

Com. Bishop Njoroge: Thank you very much. Tungetaka kuwapatia wanafunzi kuzungumza kabla hawajarudi shule na nitawaita nikianza na Shadrack Ngirisho, nikikuita unakuja haraka kwa sababu ya wakati wetu Shadrack kutoka Rombo Boys.

Shadrack Ngirisho: Nimeshukuru, mimi ni mwalimu na nitazungumza tu kwa ufupi na nina mambo kadhaa.

Langu la kwanza ni kuhusu haki ya mwana ama mtoto. Naona kwa Katiba imeelezwa kwamba, mtoto ama mtoto ana haki zake za kulindwa. Ningependa tu kuzungumzia kuwa Katiba iangalie, haki za mtoto kama ni elimu, apata elimu ya bure na

watoto wa kike ama wa kiume wawe na haki sawa.

Masilahi ya wanawake: Kwamba imeandikwe ihakikishwa kwamba mahitaji yao yameakilishwa kikamilifu. Ni kwamba labda katika sehemu nyingi haki za wanawake zinanyanyaswa, labda watoto wa kike wanakosa haki ya kupata nafasi ya kusoma kwa ajili ya tamaduni zetu ama kwa ajili ya hisia tofauti ya wazazi. Ningependa kwamba Katiba ihakikishe kwamba, maana kuna watoto ambao wanataka kusoma na labda haki zao zinadhulumiwa, wazazi wanakataa labda kuwapatia nafasi katika hali ya kusoma. Ningependa kusema wale viongozi ambao wanahusika, labda mtoto anataka kusoma amepeleka labda maoni kwa viongozi. Ningependa tu kusema viongozi wawasaidie, viongozi wa utawala wawasaidie, ili waweze kupata haki ya kusoma.

(Interjection)

Com. Bishop Njoroge: Tumepata hiyo, hebu nenda kwa pointi ingine.

Shadrack Ngirisho: Hayo point ingine ni haki ya ajira ama chakula na makazi. Tungependa labda nayo sheria ihakikishe kwamba wale wanaosoma wasiwe wanasoma kwa bure, sheria iwapatie nafasi ya kupata kazi na pia kama ni shuguli ya kupata nafasi katika colleges nazo sehemu hizi ziangaliwe. Kuangalia kwamba watoto wanaosoma wapate nafasi katika colleges hata kama ni sehemu za Army katika serikali nao wapate nafasi waende wasome taaluma tofauti.

Ya mwisho ni Katiba ilinde haki ya walemavu, labda tungeomba serikali nayo katika hali ya kutafuta maoni, ipate kuanzisha Special Institute hapa, nao watoto watu wale labda hawawezi kusikia na wale hawawezi kuona wapate haki ... (incomplete).

(End of Tape 2, Side A)

Irene Lempila: Kwa nija naitwa Irene Lempila, maoni yangu ambayo ningependa kupeana kwa Tume hii ni kwamba nafasi ya maskini na tajiri imeendelea kuwa kubwa sana na ningetoa maoni ya kwamba wanapounda hii Katiba wahakikishe ya kwamba umaskini umejaribiwa kupunguzwa kabisa. Yule mwananchi maskini, serikali itenge kiasi fulani cha pesa ambacho yule mwananchi ambaye hajafanikiwa kupata kazi kubwa aweze kujiendeleza nazo. Kwa sababu tusipotengewa pesa kama hizo hata kulipa hospitali itakuwa ni vigumu sana na kama hawawezi kutenga pesa kama hizo wahakikishe ya kwamba yule mwananchi wa chini kabisa anaweza hata kuhudumiwa hospitalini na hata kuenda shule. Kwa hivyo ingekuwa ni vizuri kwa Tume hii ama Katiba ilinde hali ya mwananchi mdogo kabisa. Asanteni.

Com. Bishop Njoroge: Thank you very much. One minute?

Com. Lethome: Mwalimu nilikuwa natarajia utazungumzia habari ya haki ya mtoto wa kike na mila ya Kimaasai. Umesemaje habari ya kurithi?

Mrs. Lempila: Kulingana na urithi wa msichana wa Kimaasai, mimi ningependa iwe automatic, iwapo tu labda hajaolewa.

Isijalishwe kwa sababu nilikuwa nimesikia mzee mmoja akisema ya kwamba hao ambao wamekosa matumaini ya kuolewa, iwe automatic hata kama ujafikisha umri upate nafasi ya kurithi mali ya baba yako, hiyo isiwe determining factor kusema ati ukifika umri fulani ndio utajulikana. Baba akifa kabla hujafika umri wa kuolewa na hutaolewa hutapata kurithi, kwa hivyo mimi ningesema ya kwamba msichana awe na haki ya kurithi hata kama ameolewa.

Com. Bishop Njoroge: Asante sana mwalimu. Tupate Saud Mohammed. Tuambie miaka yako na darasa lako.

Saud Mohammed: Kwa majina naitwa Saud Mohammed niko darasa la nane nina miaka kumu na mbili. Maoni yangu ni kwamba, swali la kwanza ni Katiba ni nini? Kila siku nasikia tu kwa radio Katiba lakini sijui ni nini?

(Interjection)

Com. Lethome: Kwa hivyo ungependa tukueleze Katiba ni nini?

Saud Mohammed: Ndiyo.

Swali la pili ni kwamba, Katiba hii inafaa ifundishwe katika shule kuanzia darasa la kwanza hadi la nane.

Swali la tatu ni, ni nini inayorekebishwa katika Katiba na kama inarekebishwa kwa nini wanachukua siku nyingi kurekebisha.

Ni hayo machache.

Com. Bishop Njoroge: Very important questions and they have to be answered. Karibu sana Mohammed. Mparanat Logela, utuambie miaka yako na darasa lako.

Mparanat Logela: Niko katika darasa la nane na nina miaka kumi na tano.

Com. Lethome: Jina?

Mparanat Logela: Mparanat Logela. Swali la kwanza, wazazi wanapokataa kuelimisha watoto, serikali inachukua jukumu kuwasomesha.

Swali la pili, sisi tukiwa wanafunzi sioni haja kusoma kwa sababu wengi wamesoma lakini hatuoni kitu wanachofanya. Kwa hivyo ningependa tu kusema. Kuwa lazima tuzingatie elimu yetu la sivyo tutarudi na kulima mashamba yetu au kufanya bishara na vitu vingine. Ni hayo tu.

Com. Bishop Njoroge: Thank you very much. Anasema angeliitaji kazi akimaliza masomo. Si ni kweli? Karibu hapa.

Tupate Wanjiku Njuguna.

Wanjiku Njuguna: Kwa jina ni Esther Wanjiku niko class eight na niko na miaka kumi na tano. Maoni yangu ni hivi, sisi wanafunzi hatuoni sababu ya kusoma kwa sababu tunapoangalia tunaona kwamba watu wengi ambao wamesoma hawajapata kazi wala hawana matumaini ya kupata kazi. Kwa hivyo hata sisi tukisoma tutarundi nyumbani ili tulime, kwa hivyo tunaomba mtuandalie kazi.

Ya pili, elimu ya msingi tuwe tunapata bure kama zamani kwa sababu wazazi wengine hawana uwezo wa kulipa karo na hata wengine hawapati pesa za kununua vitabu, kalamu na hata kununua uniform.

Ya tatu, siku hizi wazazi ndio wanao waajiri walimu nchini kwani walimu ambao serikali imeajiri hawatoshi, hivyo sasa wazazi ambao wamewalea watoto ndio wanaopewa mzigo mwingine wa kuajiri walimu. Ni hayo tu.

Com. Bishop Njoroge: Thank you very much. Si mnaona Katiba ni muhimu sana hata watoto hawaogopi. Si ni kweli? That is very nice, I do not know whether Bwana DO uko tayari, karibu.

Maalim Mohammed (DO): Shukran, mimi sikuwa na maandishi bali niko na maoni moja ama mawili ya kupeana. Kwanza vile mlivyojulishwa kama wananchi, tunawahakikishia kuwa maoni yale mtapeana hapa ni haki yako, tukiwa na mheshimiwa ama mimi DO nikiwa hapa hatuna mamlaka ya kuuliza mtu yoyote swali kuhusu maoni yako vile ulivyosema. Kwa hivyo una uhuru na kama ni kusema hata juu ya DO wa Loitoktok, tafadhali sema.

Com. Bishop Njoroge: Bwana DO can you tell us your name?

Maalim Mohammed: Kwa majina naitwa Maalim Mohammed vile wananchi wengi wanavyojua, mimi ni DO wa Loitoktok na nashukuru kupewa hii nafasi.

Yangu ya kwanza ni mambo ya usalama. Nataka iwe wazi katika Katiba yetu ya kuwa, mara kwa mara jina la serikali linachafuliwa kwa sababu ya ukosefu ama kwa sababu ya laxity fulani kwa maofisa wanaohudumu katika hiyo sehemu. Kwa hivyo ningetaka iwe wazi ya kuwa katika Katiba yule DO ako katika sehemu pamoja na OCS. wale maofisa wengine wawe na jukumu la kuhakikisha usalama wa wananchi. Lakini, ningesema on condition there are the resources available to them. Nafikiria wananchi wanaweza kushuhudia katika sehemu ya Loitoktok tuko na zaidi ya kabila arubaine na mbili ambao tuko nao Kenya lakini kwa sababu ya ushirikiano wetu na kwa sababu ya ukarimu wa jamii ya Wamaasai hatujawahi kuwa na shida, vurugu inatokea mara kwa mara lakini tukiongea tunasuluhisha na tunakuwa na amani. Tunashukuru Mwenyezi Mungu na tunashukuru Wamaasai.

Ingingine ni mambo ya human wildlife conflict. Nafikiria hii ni jambo la kufikiria, kila Maasai hapa ameguzia na wataendelea kuiguzia. Kumekuwa na binadamu kuwawe na wanyama wa pori, kumekuwa na umaskini kuletwa na wanyama wa pori kwa sababu wananchi wamefanya bidii kuhakikisha wanapigana na umaskini, wametengeneza mashamba, wamepanda chakula kwa wingi lakini kwa siku tu ndovu anatokea na ile ekari tano umepanda inafagiliwa. Na vile tunavyojua katika hiyo Act, hakuna compensation katika property ama damage ile inatokea katika crops zetu na pia ile malipo binadamu analipwa na serikali yetu akikufa, hiyo nafikiri naweza kusema ni negligible. Kwa sababu kulipa binadamu elfu thelathini, hiyo sio binadamu, tumesema serikali kupitia katika hii Katiba lazima hiyo irekebishwe. Kama vile Wabunge walivyoongea wakati fulani wakapitisha Milioni moja, inafaa kutekelezwa. Na pia kukiwa na damage ya crops ama any other property, the concerned parties kama Agriculture wawe wanafanya assessment na wanapeana recommendation yao na hiyo ni lazima serikali ione ime-compensate huyo mwananchi.

Jambo lingine ni mambo ya ardhi. Nafikiria katika sehemu ya Masaaini ama wachungani kwa jumla, bado hatujajua umuhimu wa ardhi ingawa tumejaribu juu na chini kuwaelemisha. Na kwa sababu ya utamaduni wetu sisi, nikiwa Msomali kwa mfano, ukiwa Maasai, tumesema sisi hatuwatambui akina mama. Lakini kupita hii Katiba tunataka kusema namna hii, ardhi iwe inamilikiwa na mzee na mama. Ndio tufunge hii loophole ya labda kuna corruption katika Land Control Board ndio inafanya labda kupitisha shamba bila idhini ya mama. Lakini tukiwa na majina yote katika hiyo title deed, itahakikisha mama amekuja na watoto na wame-sign application wote. Kwa hivyo ndio unasikia mara kwa mara Land Control Board Chairmen tunalaumiwa kwa sababu kweli kuna loophole na sisi wenyewe kama binadamu we take advantage, although not all of us do that.

Jambo lingine ni mambo ya elimu, hii ni maoni yangu ndungu zangu Wamaasai. Mambo ya elimu bado tuko nyuma sana sisi wachungaji, ingawa kumepitishwa kupitia Bunge letu ile kitu tunaita Children Act, bado haitilii maanani ama itupatie uwezo kamili ni nini tunaweza kufanya kuhakikisha masomo yamepeanwa. Kwanza kabisa itakuwa ni maoni yangu kuwe na free and compulsory primary education.

Ya pili, ndio sisi wachungaji kwa sababu pia wazazi wetu huko nyumbani sehemu ya North Eastern wanafanya kitendo kama hicho, tuhakikishe yule mzee ako na mali, Machifu na wazee wamepewa mamlaka wanauza mali yake ili kuhakikisha huyu mtoto amepata karo ya kusoma katika secondary school.

Mambo ya msichana, nafikiria hapa imekuwa ni nyimbo. Msichana akifika darasa la tano ndio huyu amezwa bwana amepewa. Kusema ukweli Machifu wa hii sehemu wamefanya kazi mzuri wakishirikiana na Madiwani na waalimu kuhakikisha hawa wasichana wameokolewa na lobby groups hasa nawashukuru. Kwa hivyo kuwe katika Katiba mambo fulani hata kama ni fine ama kuna uwezo wazee wanapewa kuhakikisha huyu mtoto ameokolewa na anaendelea na masomo yake.

Jambo lingine ni kuhusu mambo ya urithi, nafikiria tunataka iwe ni haki ya kila mtu, msichana pia apewe kama binadamu mwingine haki ya kurithi mali ya wazazi. Na katika kurithi pia kuna jambo nataka irekebishwe, tumekuwa na mambo ya

taxation, unasikia mzee amekufa watoto na mama wamebaki na wanaambiwa mpaka mshtaki kifo ndio labda mtagawa hii mali yenu. Lakini jamii kama hawana shida, why should they be given that burden kuhakikisha wanachukuwa advocate certificate, wanaenda mpaka High Courts, that is very inconveniencing. As long as there is an agreement within that community or the family, tunataka hiyo sehemu iangaliwe.

La mwisho, sisi tukiwa Waafrika, nafikiria kabla sisi kuletewa hii mambo ya sheria na wakoloni na ingawa tumeshirikishwa Wakenya, tulikuwa na utamaduni wetu. African Customary Law ya kusuluhisha mambo mengi ya kinyumbani na nafikiria wakati huo uhalifu ulikuwa ni mdogo. Si ni kweli? Huo uhalifu umezidi kwa sababu there is a lot of corruption, somebody buys justice because he is well off. Hii sasa imekuwa ni kiwango, mwananchi wanadaiana madeni, Chifu anawaita kwa ofisi kusuluisha hilo jambo. Yule ana uwezo anakimbia kwa advocate, Chifu anakuja kuuliza wewe umekuwa, recovery dept institution. Je, huyu mzee anajua High Court iko wapi? Na anadai mwingine shiling elfu ishirini. Kwa hivyo, kwa hayo machache nasema asanteni, Mungu awabariki.

Com. Bishop Njoroge: Bwana kuna maswali.

Com. Lethome: Kuhusu mambo ya security, umesema kuwa officers ama wale wanahusika na mambo ya usalama waweze kupewa facilities za kuwawezesha kufanya hiyo kazi. Ningependa tu uzungumzie kidogo kuhusu terms of services on security personnel. Zungumzia habari ya Polisi whether regular or the APs, do you think under the new Constitution we need to review their terms of services because you cannot expect mtu ambaye ni frustrated akupatie security.

Maalim Mohammed: Thank you. Nafikiri Bwana Commissioner Lethome hilo ni swali nzuri. Nafikiria tukisema resources za kuwawezesha mtu kufanya kazi yake ni mingi. Ingawa mambo ya usalama Bwana Commissioners nafikiria siwezi kuingilia ndani zaidi kama mfanyakazi wa Serikali lakini ningependa, terms of reference is an important issue, facilities pia na mambo ya simu, mambo ya gari na mambo kama hayo pia inaweza kutuawezesha. Kwa sababu tukiwa na jambo la dharura, ni lazima uwe na gari na mafuta karibu ndio uweze kukimbia hiyo sehemu kuokoa maisha ya wananchi.

Com. Bishop Njoroge: Asante Bwana DO nimekuwa huko upande wa Samburu mahali panaitwa Baragoi, unaona hata DO hana gari kwa hivyo shida ikitokea, DO hawezi kufika mahali kuna shida na kwa hivyo DO ni lazima Katiba imshugulikie. Ningetaka kukuuliza swali moja au mbili. Nataka kusikia, umesema kwamba unataka Katiba iweze kufanya kwamba kila mzee aliye na title deed iandikwe mzee na bibi yake. Hivyo ndivyo ulisema?

Jambo la pili ni kwamba, umesema wasichana wasiolewe kwa nguvu au kabla hawajamaliza masomo. Ungetaka ku-propose age ya msichana kuolewa iwe age ya ngapi ili akubaliwe kuolewa na wakati huo mwingine awe shule?

Maalim Mohammed: Nafikiria mambo ya kuolewa Bwana Commissioner, kila jamii wako na mila na desturi yao lakini yangu

hasa nilikuwa naonea kwa mambo ya elimu. Yaani kuna nadhamu ya wasichana kutolewa shuleni wanapewa “sugar daddies”, wazee kupita umri hata labda ambayo hataweza huyo msichana. Kwa hivyo msichana angepewa nafasi amalize masomo yake na pia choice yake, yule bwana atampenda si hii mambo ya kulazimisha. Asante.

Com. Bishop Njoroge: Asante sana Bwana DO uta-register pale. Mheshimiwa karibu.

Geoffrey Paipai: Bwana Commissioners nafikiri mtaniruhusu kuchukua muda mrefu kidogo kuliko wenzagu kwa sababu mimi nawakilisha...(Inaudible).

Kwanza nataka kusema ya kwamba.....

(Interjection)

Com. Bishop Njoroge: Anza na majina.

Geoffrey Paipai: Jina langu ni Geoffrey Nepukoi Paipai, Mbunge wa Kajiado South,. Nikitoa maoni ya vile Katiba ningependa irekebishwe iweze kusaidia Kenya mzima na watu wetu hapa.

Ningependa kwanza kuzungumzia ni serikali aina gani tungelipenda kuwa nayo katika Kenya? Maoni yangu ni kwamba, serikali tunayotaka kuwa nayo, ningelitaka nione Kenya ikiwa nayo ni ile Unitary Government. Kwa sababu tukiwa na hii tunaita Majimbo, sijui jina gani lingine, hatuelewi tutaweza kuwa na Majimbo namna gani na nchi hii vile iko maskini na tunajua tukianza kuzungumza habari ya Jimbo na nini tutakuwa tunaongeza gharama katika kule kugawa gawa Kenya vile inatakiwa. Iteleta tena uadui kati yetu, tutaanza kusema Jimbo itafika wapi? Akina nani watakuwa katika ile Jimbo? Itakuwa lini? Hizo zitakuwa ni gharama zaidi na si kwa manufaa ya nchi hii wakati huu. Kama tumesema tunataka Unitary Government ningelipenda kuzungumza kuhusu structure, serikali ile nimesema ya Unitary. Sasa hiyo serikali itakuwa namna gani kutoka juu mpaka sub location.

Ningependa kusema hiyo serikali ningelipenda kuona ikiwa na Rais, Rais ambaye ana limited executive powers. Because President ndio unifying factor ya serikali, lazima kuwe na baba, kila boma lazima iwe na baba, so President awe ambaye ana-powers kiasi fulani halafu Vice President vile vile awe ambaye atakuwa deputy wa huyu President. Halafu hapo chini tuwe na Prime Minister ambaye ndie atakuwa mkubwa wa serikali. He is going to be actually the head of the government.

Na huyu President ningelitaka achaguliwa namna gani? Huyu President ningelipenda achaguliwe na wananchi na Vice President vile vile achaguliwe na wananchi lakini atakuwa running mate isitokee msigo kama huu tunao sasa, ati kama President anaamka usiku anasema amekasirika na vice wake, toka. Iwe ni wananchi ndio wanaamua, siku ile President anachaguliwa watamaliza term pamoja, wajadiliane wazungumze pamoja, wasipozungumza awe hapo hapo kwa sababu ni wananchi walikuwa

wamemchagua. Na President akifa ua aondoke au atoke kwa njia yoyote, huyo Vice President ambaye ni running mate amalize ile term ya miaka tano ya President. Hakuna haja ya ku-subject nchi waende katika election na kuna Vice President ambaye wananchi wanampenda, wamemchagua. Kwa hivyo amalize ile term ya President, that way nafikiri itakuwa mzuri na wananchi hawatagharamishwa.

Huyu President anapochaguliwa ningependa kusema kwamba lazima apate kura 25% katika province tano, is a good one kwa sababu utaonekana vile umekanyaga kanyaga katika Kenya. On top of that, lazima awe amepata zaidi ya kura 51% ya kura zote ambazo zimepigwa wakati huo. It is not enough mtu akipata kura 30% au 20% na tusema amekuwa President kwa sababu ana kura mingi, that one is not enough, he must ganuer 51% ya zile votes ambazo zimepigwa Kenya mzima. Kama kwa bahati mbaya wote wamepata hawajafikisha 50%, iwe na run off. This time ikiwa na run off, yule atakayepata majority votes hata kama ni 20% au 30% but number one and two wafanyiwe run off. Yule atakayepata kura mingi than the rest, ile rule ya kusema 25% or whatever tusifuate, tufuate yule atayekuwa na kura mingi. That way we shall have a President who is popular and a President who is capable of running this country.

Tunataka huyu President ambaye yuko, kwanza awe Mkuu wa Majeshi, that is duty that the President will have hata kama tunamwondolea powers lazima awe Mkubwa wa Mjeshi. Lazima huyo President awe ndio Chairman wa Cabinet and he is also bound by collective responsibility. Huyu President lazima naye awe ndio anahusika na meneno yetu ya nje. Sikusema ati nataka awe Minister for Foreign Affairs. What I am saying ni lazima hata kama kuna Minister of Foreign Affairs, he must have a hand in that ndio akienda nje kuzungumzia sisi ama akienda kwa niaba ya wananchi awe anaelewa na he has a say and he has some Constitutional responsibility.

Katika public functions the President has also be to be there despite the fact that we are having a Prime Minister who is the head of the government. Kwa hivyo tukiwa na President wa aina hiyo then I think it will be his duty to run this country effectively with a lot of respect. The Vice President even if he is his deputy for any other duties, anaweza kumpea Ministry .

The Prime Minister, tunataka aingie katika Constitution, hatutaka Prime Minister ambaye atakuwa kama yule wa Tanzania au wa Uganda ambaye anaweza kutolewa hana mamlaka, tunataka aingie katika Constitution. Huyu Prime Minister atachaguliwa na President na ile party ambayo imepata uwingi wa Wabunge Bungeni katika election. The Prime Minister atakuwa mkubwa wa serikali, ndiye atachagua Ministers, ndiye atachagua all constitutional officers hata zile zingine ambazo si contitutional offices yeye ndiye atachagua. The only rejoinder to that is that this Prime Minister ni lazima achukue majina apeleke katika Parliament, Parliament will have a vetting Committee ambayo itajua au itaangalia hayo majina waone kama hawa watu wanafaa kupewa au hawafai kupewa.

Ya mwisho inatoka katika ile committee ya kazi, that way nafikiri distribution itakuwa mzuri, itakuwa inachukua wale watu ambao ni capable. This way we shall not have illiteracy among in heads of parastatals and other bodies. Kwa hivyo tutakuwa

na hawa, tumezungumza habari ya Prime Minister as the head of government pia appointments tumezungumza na ningelipenda kusema sasa tuna serikali tumetengeneza structure, tumekuwa nayo, appointment tumesema ni akina nani watakuwa appointed sasa tunaingia katika powers zile ambazo tungetaka Constitution ya sasa inyanganye President ndio President awe President, mzaliwa mpya.

Ya kwanza tunataka Section 23 of the current Constitution ifutuliwe mbali, hiyo section inasema kwamba ata kila mtu akiwa nchi hii akifanya kazi unafanya kwa sababu President anapenda ufanye. Hatutaki apende tufanye kwa sababu hata yeye tumemwaandika. Tunataka tuwe tuko huru kwa sababu sisi ni wana Kenya na sisi pia tuko kama yeye, kwa hivyo hiyo section ifutuliwe mbali. Tunataka vile vile Section 58 and 59 of the Constitution ifutuliwe mbali mahali ambapo hiyo section inasema namna President anaweza kuamka pia aseme Bunge imevunjwa, tunataka katika Constitution iwekwe tarehe ya kupiga kura, ukiingia tarehe kumi unajua utatoka tarehe kumi na tano. That way I think we shall have an organized Parliament and members would know when and how to organize their programme.

Tunataka tena katika Constitution mpya iwekwe section ambayo itafanya President awe censured, akifanya makosa aweze kuulizwa, iwe namna hata kama kumuita au vote of no confidence au nini iwe katika Constitution. We need to have a President who knows that he can be called upon to answer whatever mistakes he makes. Hiyo ndio ningependelea President anyang' anywe hizo powers.

Nitakuja sasa kwa Local Authority, hii serikali ingine ningependa nguvu ya serikali iteremshwe ije katika Local Authority, we want a powerful Local Authority. Tunataka Local Authority irudi mahali ilikuwa wakati wa 1960 mpaka 1970, wakati Local Authorities were running roads, health, water, tunataka waanze kufanya hizo kazi. Ikiwa ya kwamba Local Authority ndio inatutengenezea barabara, ndio wanatutengenezea hospitali, itakuwa rahisi because management ni hapa na wale wananchi ambao watahudumiwa ni hawa hawa hapa. Hatutaki budget inatengeneza Nairobi na hatujui nani anatutengenezea na haifiki kwetu. Ili waweze basi kufanya kazi hii ambayo tunasema wapewe tunataka percentage fulani ya national budget wapewe Local Authority specifically for those services ambazo tunataka wa-run katika areas ambapo wako.

Ili nao hawa waweze kutekeleza hilo jukumu ambalo tunawapatia, tungelitaka Local Authorities wapewe powers. The Minister, yule Minister wa Local Government, Act imepatia Minister powers za kufanya kila kitu. Everything is being refered to the Minister. We should limit the powers of the Ministers such that majority of the decisions are made by the Councillors themselves and this is why we are saying we are making Councillors Executives and if we are making Councillors Executives so that they decide and execute, then their qualifications should also rise to that of Form four for them to be able to handle that, hiyo kazi ambayo tunawapatia.

Sasa tunaingia katika Provincial Administration, mimi nataka provincial administration to be scrapped from top to bottom and those services be transferred to the Local Authority.

(Interjection)

Speaker: Inaudible.

Geoffrey Paipai: Nasema nataka hii kazi kuanzia PC kuenda mpaka Assistant Chief zote zitolewe na hiyo kazi ambayo wanafanya iwe transferred to relevant ministries. Kwa sababu kama sasa DC ndio Chairman wa District Security Committee na tuna OCPD, OCPD ndiye ashike hiyo kazi ya security. Kama ni Chairman wa education, kuna District Education Officers, achukue hiyo. At all levels mpaka Chief, so what I am saying ifanywe and this time round tuwe na structure kusema ya kwamba tuwe na district na Council at provincial levels, hiyo provincial administration haina kazi even in the current system the people do not refer to the provinces so provinces should not be a subject ati tuna centre a lot of things at the provincial level.

Hawa ambao wanaitwa Administration Police warudi kwa ile title ilikuwa zamani wawe local, initially walikuwa wanaitwa tribal Police but this time instead of calling them tribal Police we should look for a better name wawe Local Police because we want them to be under Local Authority. They are the ones to be used by the local councils to collect revenue and of course give them powers to be able to function effectively. One would wonder, nani atasimamia kazi ya district badala ya District Officer, badala ya Chief. Chief wakati huu ndiye anasimamia mahali Councillor anasimamia so that is duplication so Councillor atakuwa hapo, we do not need two people doing the same thing it is duplication. Tukifika division tutakuwa na the community in that division wanaweza kukaa chini na wachague among the Councillors one of the Councillors ndiye atakuwa ana-chair watu wakienda kwa mikutano.

National budget: Nasema ile budget tunasomewa kila siku, tunataka percentage fulani iwe inakuja katika constituency. Nimezungumza habari ya percentage fulani iende kwa Local Authority, percentage fulani iende katika constituency. Apportionment of the national budget ije katika constituency ili wananchi waulizwe waseme wanataka nini. Kama ni milioni kumi au ngapi, iende katika constituency wananchi katika hiyo constituency waseme priorities yao hapo waweze kuendelea na kufanya vile wanaweza kufanya. This is happening in Botswana, Ghana and is happening everywhere and indeed hiyo tu ndio inawezekana, unaona Botswana ni nchi ndogo na ndio tajiri Africa. Kwa hivyo tunataka iwe hivyo wananchi ndio wanaamua vile watafanya.

Hii ni constituency yangu na constituencies zile ziko sawasawa na yangu hasa zile ambazo ziko arid and semi arid. Hizi constituencies ya wafugaji hasa ambao wanaishi mahali kame wao wana hama hama. Na njia tu ambayo inaweza kuwasaidia waweze kuwa sawa na wananchi wenzao ni kama kutakuwa na ile inaitwa Affirmative Action kwa maneno yao au kuwe na njia ya lazima ili waweze kusukumwa wakute wenzao. Kwa sababu Constitution ya sasa imetuchukua kama wote tumeanza mahali moja kukimbia ati tumewachwa nyuma na tunalanza pamoja. Tunataka tukimbizwe tukute wale ambao walikuwa mbele kabla ya Constitution hii haijakuja.

Tunataka affirmative action ambayo baada ya zile mbile ambayo ni national ambazo constituency na kila region na county Council wapewe some percentage katika budget ya kukimbiza areas hizi ambaz zimeachwa nyuma. Na hizo sehemu ambazo zimeachwa nyuma ni kama masomo, health services. Hasa kwa masomo hatuzungumzi tu ati shule iwe ni ya lazima na iwe ni ya bure, mimi nakubaliana na hiyo lakini lazima nayo iwe na mobile schools. Kuna communities ambao wanahama and they have no choice, lazima wahame kwa sababu ukame umeingia, waalimu wahamishwe, wawafuate na shule iwe erected kwa sehemu za zenye zina maji and allowances be made available. Hiyo ndi sababu nazungumza habari ya ile percentage ya pesa iwekwe katika hiyo na hata hospitali iwe na mobile clinics ambayo inafuata wao na iwe parmanent wakirudi nyumbani wakati imenyeshwa wakute kama permanent clinics ziko.

Hata katika kazi, lazima kuwe na namna ya kuhakikisha ya kwamba watoto wa watu ambao wametoka hizi disadvantaged areas, hawa watu ambao wameachwa nyuma kwa sababu ya geographical situation hapa waweze kuwa wanapewa incentive. What I am saying ni kwamba hii affirmative action iweko na iwe backed na zile pesa ambazo zinapeanwa kwa sababu bila pesa hawawezi kufanya chochote.

Tuende katika Mashamba, hii habari ya mashamba, we have a problem because tukizungumza habari ya Land Control Board, kama vile mimi najua na vile naona inafanyika hii haifanyiki kwa haki, sheria haifuatwi. It is not the law that is defective, si sheria ndio mbaya lakini watu wame-flout sheria, serikali ndio ime-flout sheria. Sheria inasema ni Council na wazee ndio wanakaa katika Land Board lakini Provincial Administration imechukuwa ati wao ndio wanakaa katika Land Board. Infact what is even happening today is illegal, kwa sababu sheria haijazungumza habari ya DC, haijazungumza habari ya DO, imezungumza habari ya Council na wazee. So we want to put some weight ya kwamba sheria ifuatwe so that such a law iwekwe kwa sababu sheria ndio inavunjwa. What has been happening all along is illegal because the law does not talk about Provincial Administration, it talks of Council na Wazee. Kwa hivyo hiyo inatakiwa iwekwe mkazao irudi mahali inatakiwa.

Kwa wale ambao wanauza shamba I totally agree with the DO, shamba ukishapewa hii ni yako, kwa sisi ambao hatujui maneno mengi. We are talking of freehold, leasehold hiyo ni tofauti mtu aandike jina lake auze, afanya vile anataka. Lakini kwa hii freehold wacha shamba iwe ni ya familia, (family land), iwe kwa jina la mzee, la mama na hata mtoto akifika 18 na ni wa huyo mzee aandikwe so that namna ya kuuza iwe ngumu, mpaka kuwe na mkutano nyumbani ya kutosha watu waamue kuuza. Na iende katika Land Board ambayo tunasema ni wazee na yule Councillor wa hiyo area akifanya makosa afutwe wakati wake ukifika, si kwa Provincial Administration.

Zile plots ambazo zinapeanwa na Council, hiyo nayo ni makosa. Tunasema hivi, hii plot Councillor anapeana ni ya wananchi wanishika on trust na trustee hawezi kuwa mkubwa wa nchi ambayo si yake. It is not Council land, hiyo ni shamba ya hao wananchi. Tunasema hivi, kama kuna plot iko katika area ambayo imeandikwa jina la Council na ina-hold kwa trust ya wale watu, wakati wanataka kupeana lazima waje ku-consult wale wenyewe. Na kama ni kupeana iwe advertised na wale ambao wanakubaliwa kutuma maombi wawe ni wale wenyewe.

Kama ni Rombo, ni Wanarombo ndio watafanya application si watu watoke Loitoktok waje Rombo wangojee mahali pao wapate huko, when it comes kwa hii mashamba ya plots. Council should never sit in Kajiado na kupeana shamba ya Loitoktok, Merweshi, Matimba it should be wale wananchi wako hapo watafute na isipeanwe bila hawa kupeana ruhusa. They should also explain kwa sababu haya mashamba wakati ambao yalikuwa yametengwa yalitengwa kwa jambo moja au lingine na kama inatokea kwamba inapeana kwa sababu hiyo ingine, they should come back to the people, waambie tulikuwa tumeamua hivi. That should be the case.

Ikija kwa ile ambayo ni ya serikali, unajua kuna shamba ya serikali na kuna shamba ya Council. Shamba ya serikali, hiyo sasa tunasema hivi, President asiwe na ruhusa ya kupeana Commissioner, he should not be allowed. Sheria iandike katika Constitution that, that is one of the responsibilities ambayo President au Minister amenyanganywa, iwe ya wananchi. Ikiwa kama ni ya kupewanwa, advertisement iwekwe, not only in the Kenya Gazette kwa sababu wananchi hawaoni, iwekwe kwenye Kenya Gazette iwe legal na iwekwe katika Local dailies ili watu wote wajue ya kwamba kuna shamba linapeanwa Garissa ama Nairobi ili kila mtu apate Nafasi ya ku-apply. Lakini isiwe ati kuna mtu moja anajua mwingine hajui halafu watu wanapewa bila sababu. Kwa hivyo, hiyo tunataka iwe hivyo. Kwa forest tusikubali kabisa, forest to remain the way it is na hiyo ni lazima iende Parliament if any land has been set aside.

Halafu nomination....

(Interjection)

Com. Bishop Njoroge:(Inaudible)

Geoffrey Paipai: I want more time, I am about to finish.

Nomination: Mimi nataka nomination iweko, nomination ya Parliament na Council iendelee tu kama vile sasa isipokuwa this time round wale wale nominated, sheria tu haifutwa because it should be for special interest groups, mtu akichaguliwa na ha-represent special interest groups, huyo iwe challengeable aweze kutolewa ili tupate proper nomination. Hatuwezi kusema tunatafuta special interest na tukiingia huko labda tunataka akina mama, mama hayuko, labda tunataka tupate disabled na hakuna. So, kuwe na Clause katika Constitution ya kusema, if nomination is done and does not represent special interests that should be challengeable. In other words there must be a memo on every nomination, that you are nominated, Paipai is nominated because he represents one, two or four things. That should also apply to the Council nominations.

Nataka kama Commissioner of Police, that office ya Commissioner of Police iwe Constitutional kwa sababu security katika nchi hii imekosekana kwa sababu that office is not independent, anaweza kutolewa leo, anaweza kutokuweco kesho so we

want that office iwe a constitutional office, other offices wasiwe lakini yeye awe.

Judges: tunataka every appointment ya Judge be vetted by Parliament, the Judge and above, Magistrate anaweza kuchaguliwa na Commission lakini hiyo ingine iwe vetted by Parliament.

Human rights ambayo ndio ya mwisho, girl child hasa pastoralists inatakiwa tuwapatie nguvu kidogo kwa sababu ukijaribu kuona wasichana wetu wa pastoralists hawasomeshwi na hiyo ni discrimination. Tunataka msichana apewe nafasi katika education, kwa hivyo kila mtu asome lakini girl child apewe nafasi ili aweze kupata kusoma.

Security, the government should actually guarantee security not by word lakini ionekane kwamba inafanyika. Asante.

Com. Lethome: Kuna maswali. Swali la kwanza ni kuhusu kazi ya Wabunge kama Mbunge leo hii unaona kama Wabunge wamepewa nafasi na facilities ya kuweza kukutana na wale walowachagua katika sehemu zao za wakilishi? Kama hapana, unapendekeza kitu gani? Unapendekeza nini kuhusu nani atakayeamua mishahara au marupurupu ya Wabunge na je ikiwa Mbunge amechaguliwa na hakuweza kuwakilisha watu wake inavyopasa, ungependa hawa watu wangoje mpaka miaka mitano iishe au wawe na uwezo wa kumuita na kufanya uchaguzi tena kabla ya miaka mitano kuisha? Asante.

Com. Bishop Njoroge: Nataka kuongeza ili ujibu yote. Mbunge akichaguliwa kwa party fulani na aende Bunge na abadilishe party hiyo katika Bunge, wewe kama Mbunge ungesema nini? Kwa sababu tunataka kuunda demokrasia na watu wakikaa waki-change parties zinakufa, hiyo ningetaka kujua. Pia habari ya security, government guarantees security. Tunaweza kufanya nini kama hakuna security, ni kitu gani tutafanya ili iweze ku-guarantee security? Kuna kiti mwananchi anaweza kufanya kama anasikia insecured kwa serikali, kuishurutisha kuwa-secured?

Com. Lethome: Mheshimiwa pole, we are going to bombard you with more questions you know you speak for many. Hivi leo, tumezunguka Kenya mzima karibu sasa, wananchi wanalalamika kuhusu brutality from those who are mandated to provide them with security. Kwa mfano, leo hii mwananchi akinyanyaswa na Chifu hana mahali pa kukimbilia, ungependekeza nini chini ya Katiba mpya? Akidhulumiwa na Police Officers anaenda kumshtaki kwa OCS ambaye ni Police Officer pia, yaani inamaana kuwa hana mahali pa kushtaki. Tuwe na ratiba ya aina then you go and report au itabidi uende mahali pengine? Je, ungependekeza kitu gani about brutality by those people in leadership position or who are entrusted with taking care of the other people? Thank you.

Geoffrey Paipai: Asante kwa maswali hayo, nataka nianze na habari ya facility. Ukweli ni kwamba wakati huu Wabunge hawajapewa uwezo wa kuweza kuhudumia wananchi vilivyo. Kwa sababu ingelitakiwa Mbunge kwanza awe na, simu na wafanyikazi, researcher na office messenger na awe na full office secretariat suit katika constituency ili mtu yoyote akitaka kuja kumwaona anakuja huku na awe na mtu ambaye anachukua messages na aweze kupigiwa simu na aweze kupiga simu. Those

facilities must be there, kwa sababu kama hizo haziko huwezi kupata namna ya kuongea na watu, lazima uwe na karani. Kama mimi nikitoka hapa saa hizi, nitazungumza karibu na nusu ya hawa watu na vile wangesema yote haiwezi kuingia kwa kichwa. Lakini ukiwa na karani ataandika chini na aseme, fulani amesema hivi na fulani asema hivi, you can be able to sit down and sort that out.

Ofisi inatakiwa hapa na inatakiwa Nairobi pia, nikiwa na shida kama saa hii nimekuwa leo kama mimi ndio nimejitengenezea hii note, kama ningekuwa na researcher, he would have done this for me, ningekuwa tu hapa tu kupeana views after goind through so a lot is required ili Mbunge aweze kufanya hayo. In terms of office, facilities, workers, researchers and all that hata internet tunataka tuwe tunazungumza. Si ati kwamba Mbunge, mtu wangu akitaka kujua kama Mbunge waku yuko Bunge anaweza kupiga simu na ajue Mbunge wake yuko Bunge. Akitaka kujua niko wapi wakati wote, he can inquire. Therefore, facilities are required, but should be at the constituency and at the national level, that is very important and is not there.

Ya pili tunazungumza habari ya Parliament, I would want to say this, mishahara ya Wabunge iwe na Tume au sheria ambayo inahusiana na mishahara ya Wabunge vile inaongezwe kwa sababu hakuna mishahara inapunguzwa hua tu inaongezwa au inakuwa reviewed. Kuna Tume ambayo inafanya hiyo kazi na saa hii tunapozungumza hiyo Tume inaendelea na hiyo kazi. Si ukweli ni kwamba Wabunge ndio wanajiongezea mishahara and I pity wananchi, today I am a Member of Parliament, tomorrow I will be out lakini hakuna namna ingine ninaweza kusema ati kuwa na extended body kwa sababu if there is an extended body, kuna hiyo Tume inaenda ina-review inaleta recommendations katika Parliament na ni kwa sababu ni lazima iwe ni sheria na sheria ni Bunge tu ndio itaweza kutengeneza lazima itarudi.

Hata saa hii tukisema itengenezwe na Judges haiwezi kuwa sheria mpaka irudi kwa Parliament, hawa Wabunge ndio watakuja kuzungumza, so it is a problem that we have to deal with. Labda kama Wanakenya wataamua which is not one of the things that I would recommend, waseme tuwe na Upper House na Lower House, labda hii ya hawa iangaliwe na hawa, but I think lazima iende kwa Bunge ndio iweze kuwa sheria. So there is no way tutasema tuwe same, it will never be and it has never been anywhere else in the world. Duniani mzima lazima iwe kwa sababu ni sheria, so there is nothing much I can say about it.

Kuhusu maneno ya Mbunge ambaye hafanyi kazi na wananchi wanaamua kumwondoa. hiyo nafikiri haiwezekani duniani na singefikiria hapa itawezekana. Kwa sababu unapoenda kwa Bunge, kama mimi niko kwa Bunge nilichaguliwa na watu, niliangalia juzi ile percentage nilipita nayo, nilipita na 66% ya wale watu ambao wamepiga kura. Kuna wale watu 34% bado wako hapa wanalalamika tu, kwa hivyo hawa wanafaa ku-pass a vote of no confidence. You, see what I am saying, hakuna namna ati Mbunge hata saa hii nikisema ni watu wangapi wanapenda Paipai kuna wale watasema hawapende Paipai. Kwa hivyo kama tutakuwa tunasikiza wale na wale hawatusikizi, haiwezekani then I think it is going to be very expensive. Kupiga kura katika constituency moja inagharimu Wakenya million thelathini na tano, so why spenda Kshs. 34 Million na hata huyo akichaguliwa kuna watu ambao watasema hawamtaki?

Com. Bishop Njoroge: Hebu niongeze hapa Mheshimiwa ili ujibu vizuri. Kuna mahali pengina kama Lodwar tuliambiwa kwamba hakuna haja kufanya uchaguzi yule aliyekuwa namba mbili achukue hicho kiti.

Geoffrey Paipai: Hiyo ni kweli lakini haiwezekani kwa sababu majority, wale wengine ambao ndio majority wanasema hata huyu hawakumchagua so there will be arguing. What I would say is that, wananchi lazima wavumilie wangojee mpaka miaka mitano, five years is not too long for one to wait rather than waiting, kama vile tunasema habari ya civil servants mpaka wanakaa mpaka wafike 55 years. So, it is going to benefit the country na hakuna wakati kelele haitapigwa.

Tukizungumza habari ya Wabunge wanachaguliwa kwa chama moja na wakiingia Bunge anaweza kuzungumza maneno tofafuti, mimi ningependa iwekwe kwa Constitution ya kwamba Mbunge akitoka nje ya kile chama ambacho kilimchagua automatically atoke kwa Bunge. Kwa sababu wananchi walikuchagua ili uende ukatekeleza masilahi au yale mapendekezo ya hicho chama ambacho kilikupeleka Bungeni. Kwa hivyo sio ati lazima uandike barua kwa Speaker, ukianza kuamua otherwise, uondoke Bunge, hiyo ni makosa.

Com. Bishop Njoroge: Na tukifanya uchaguzi kwa sababu akitolewa Bunge itafanywa uchaguzi, ataruhusiwa tena kusimama katika uchaguzi?

Geoffrey Paipai: Not that term.

Kule kunyanyaswa na tuseme na Chief, DO au Polisi hiyo inatakiwa iwe namna hii. It is true wananchi wamelia sana, unapigwa na askari hapa, unaenda una-report kwa mwingine kama OCS, hata sisi Parliament tunauliza maswali. Mtu wako amepigwa umeenda umeuliza OCS kwa hakika anajua umevunjwa mguu anasema hukuvunjwa mguu na saa hiyo imewekwe chuma na anasema hukuvunjwa mguu. Mimi nataka kusema ya kwamba lazima tuwe na Ombudman, ili kama umekosewa usizungumza na wao, unaenda kuwashtaki kwa ofisi ya Ombudsman ili aweze kuchukuliwa hatua and it is only that way may be tutasaidia kwa hiyo njia.

Com. Bishop Njoroge: Na hiyo ianze kutoka sub location?

Geoffrey Paipai: From the sub location mpaka juu and should be strengthened so that democracy irudi mara moja.

Tuenda katika security, ili serikali iweze kutekeleza sheria the government should be made liable in very many things. Kama for example nikipigwa na wakora, my family should look for redress reason from the government, waende waulize because it is their responsibility and they are paid for that responsibility. Let them sue them and they pay kwa sababu kama hawajapata mtu aliyenipiga who else would have looked for that person? Walipe, it is then that they can be able to pull up their socks na ndio tena wasipige watu wao, so the government should be made responsible. That is to say kama mtu anapatika, serikali iwe liable

to pay.

Com. Bishop Njoroge: Is it possible then tuseme kwamba kwa sababu familia zote hazina uwezo wa kifedha kushtaki serikali na kushtaki serikali inahitaji wakili. Is it then possible to allocate some money ili family hii iweza kuwa na mahali pa ku-access hiyo pesa ya kutafuta wakili?

Geoffrey Paipai: Yes, that is what I am saying that the government should have an allocation state that kama huna unaenda kushika wakili serikali inalipa so long as the..... (inaudible)

Com. Lethome: Mheshimiwa pole ya mwisho, tunakusumbua tu. Mambo ya quorum, problem ya quorum in Parliament na mambo ya technical appearance in Parliament. Unaona kama Katiba inafaa kuangalia hiyo na hii mambo ya kuwa Wabunge wanafanya kazi pengine siku tatu kwa wiki, uki-balance pia kuwa Mbunge pia anatakiwa ku-serve watu wake, je unasema nini?

Com. Bishop Njoroge: La mwisho, Bwana Mheshimiwa, tulipokuwa tukifanya 3C's, nilienda katika constituency moja Nyanza na jina tulipewa na Mbunge moja ilikuwa ya campaign manager wake, na huyo campaign manager alikuwa amekufa mwaka mzima uliopita na huyu MP hajui. Yeye ana-insist ni lazima aweko, sasa na wale Wabunge ambao hawarudi nyumbani, tutafanya nini?

Geoffrey Paipai: First and foremost quorum, tuna standing orders, hiyo singependa iwekwe katika Constitution because what has happened kama Britain ambao wana wajumbe zaidi ya mia nne, quorum yao ni ya watu watatu. Sisi hapa tuko Wabunge mia mbili na ishirini na mbili, quorum yetu ni thelathini. You see there is a difference, what I am trying to saying is kwa quorum mimi ningesema sisi wenyewe kwanza tukiwa Wabunge tu-reduce number ya quorum because when you are contributing, sio inaingia katika tape inakuwa recorded. So much that if I am interested in following what transpired the previous day, I just have to listen to taped recordings

But it is also important ili tu-address watu waingie katika Bunge ni hii maneno ya kufanya Bunge iwe televised live ili wananchi waone kama Wabunge wao wako au hayuko. Lakini maneno ya quorum should not arise because may be, sisi ndio tumeweka quorum iwe juu zaidi na ndio sababu unaona tunakosa quorum, this is why we have that problem. Lakini ikiwa televised ili wananchi waoni Mheshimiwa hajakuwa duty na huyuko katika constituency then kuna namna ya kupinga huyo mtu ili atoke. Lakini hii technical appearance, unajua there is a different debate, quorum na technical appearance. Kuna watu ambao wanafanya technical appearance, kwamba tunajua lazima uwe Bunge, kama hutakuwa Bunge for 8 consecutive sittings utatolewa.

Nataka iingie kwa Constitution ya kwamba the Speaker to restrict you, there must be a way of making the Speaker adhere to that rule because he is not adhering to that rule.

Secondly, hiyo technical appearance, kama mtu ni technical, I think there must be a way not only censuring that member but of disqualifying him because surely he is not interested. So, I would say no technical appearance ya mtu kuja na ameona ameandikwa na orderly ya kwamba ameingia, anakaa labda dakika moja au dakika mbili anaenda, na anaonekana tena baada ya 8 days. Kama kuna need to be timed, people should never be timed for them to be able to know kama kuna technical appearance au la ndio naye awe disqualified. That I would say, baada ya 8 appearances awe disqualified.

Lack of visiting the constituency, nafikiri hiyo iko na haja kwa sababu wananchi kama hawakuoni, baada ya miaka mitano, when you go back there wanakuambia Mheshimiwa si ulikuwa Nairobi tu, wewe basi baki Nairobi. Ukisema sasa in between, we shall go back to where we were, ya kwamba vote of no confidence, witch hunting itatokea na hiyo itaumiza, that is why I am saying wacha huyu mpaka baada ya miaka tano.

Com. Lethome: Lakini problem moja iko hapa, I have just come back from a place in Samburu. Wanatuambia hawajamwona tangu walimpochagua lakini wanajua mwaka huu atakuja. Tukawauliza, mtamchagua? Wakasema tukipanga mlolongo atupatie kila mtu shiling mia moja, mia moja. What shall we do tukikosa kumwona,.....(inaudible). So you see now the problem, ana-disappear for 5 years, anarudi na anachaguliwa tena. This is a problem that we need to think about.

Geoffrey Paipai: Let me put it this way, unajua wana Kenya kwa ujumla, wamezoeshwa njia mbaya ya kifedha, so much that I also know of some very rich Members of Parliament, wanakaa miezi miwili halafu Jumamosi akienda, anaeda na Briefcase ameweka hamsini hamsini, so he starts distributing mahali anaingilia constituency mpaka arudi then he disappears for another 3 or 4 months. Hiyo iko, what we need to do in our Constitution is to remove bribery from election or to make bribery an offence kwa Bunge na Council, that should be made an offence.

Com. Bishop Njoroge: Mheshimiwa I think we have taken all your views, thank you very much that you could come. Margaret Keko, tafadhali?

Margaret Keko: Kwa majina naitwa Margaret Somoina Keko. Nina maoni haya. Kwanza nitaanzia upande wa elimu. Mimi nimeonelea kwamba elimu iwe ya bure na ya lazima kwa kila mmoja kwa shule za msingi na za upili hasa kwa watu ambao wanaishi sehemu kame.

Pili, shule kwa msichana itiliwe mkazo zaidi, hiyo ni ya maana kwamba tunajua kwa hao watu wafugaji kama Wamaasai na Wasomali, huwa hawatilii mkazo elimu ya msichana. Kwa hivyo ningepia pia hata kama shule ni lazima kwa wote kwa msichana itiliwe mkazo zaidi.

Kulikuwa pia na kitu tunaita quota system kwa shule za upili na university, iko tu kwa maandishi lakini haitilii mkazo, kwa hivyo

ningeomba pia itiliwe mkazo zaidi na ninasema hasa hasa kwa watu ambao wako kwa arid na semi arid. Kwa sababu sisi tuko mbali sana katika elimu. Pia marks za kuenda katika shule za upili na university, ni maoni yangu kuwa hizo marks ziteremshwe kidogo ili pia wao wapate nafasi ya kuweze kujiunga na hizo sehemu. Kuna hizi shule ambazo zimeanza, hizi shule ambazo tunasema za binafsi, zimekuwa nyingi kiasi kwamba zinakataza hawa watoto wetu wanaohudhuria shule za kawaida kupata ile quota system. Unajua wakitumia ile quota system tunaenda kukosa watoto wa kuenda secondary kutoka shule za serikali. Kwa hivyo hizo pia ningeomba zipunguzwe na ikiwezekana basi zisiwepo.

Kitu kingine, kama ingewezekana tuwe na University kwa, kila province ama ikiwezekana hata ziwe kwa district level ili pia tuweze kuhudhuria kila mwananchi baada ya kusoma na kupata elimu. Nikiongezea hapo, tuwe na university kuu na vyou labda vya waalimu, vya udaktari na kadhalika, viwe kila mahali ndio kila mwananchi apate haki ya kumwezesha kwenda kama ni chuo ama kama ni college.

Nikitoka hapo naingilia mambo ya mashamba. Mimi kwa maoni yangu niliona ya kwamba Land Control Board iondolewe kabisa kukoka divisional level twende locational level ili iweze kuhudumia haya mambo tunasema kwamba mtu asiuze shamba. Hao watu wanajua yule mtu na itakuwa ni vigumu vile tunasema kwamba zinauzwa. Title deed, imesemekana pia iwekwe bibi, bwana na watoto, hapo ni kusema watoto ninataka kuweka msichana na ninataka kutilia mkazo. Tukisema watoto hua tunahesabu labda katika makabila mengine kwamba msichana si mtoto, kwa hivyo tunavyosema mtoto inamaanisha wote. Kwa hivyo ninamaanisha kwamba kila mtu ana haki ya kurithi kwa baba yake na kila mahali kwa sababu mtoto ana haki sawa na yule mwingine.

Kwa hivyo pia hapa kwa shamba, nimeonelea ya kwamba hii mambo ya kuuza mashamba iwekwe kwa Katiba kabisa kwamba watu wasiruhusiwe kuuza shamba lao kokote, utauza uende wapi? Kwa hivyo Katiba iwe na kipengele ambacho kitasaidia hata kama mtu atauza, asiuze yeye mwenyewe awe squatter. Kwa hivyo hiyo ningeomba itiliwe mkazo zaidi, kwa sababu tunaelewa hasa kama hawa watu wa kuhama hama, akikaribiana na mwenzake nahama, kwa hivyo atahama mpaka lini? Hiyo iwe protected, kuwe na sheria ina-protect hawa watu ya kwamba wasiuze shamba lao.

Kuwe na communal land, hiyo ninaitilia mkazo kabisa ikiwezekana hata kama ni hilo shamba likikatwa inakuwa na ile title deed communal halafu sasa mtu hataweza kuwa na yake, na itakuwa na ugumu wa kuuza hilo shamba.

Upande wa President, kwa maoni yangu ninaona apunguziwe mamlaka ana mamlaka mengi sana ya ku-appoint na kufuta. Hiyo ni moja ambayo kama inawezekana, kwa maoni yangu mimi naonelea kabisa asiwe na mamlaka hayo. Awe mtu ambaye hana constituency anasimamia. Vice President vile vile awe anachaguliwa na wananchi wote wa Kenya na asiwe na constituency kwa sababu atakuwa anatilia mkazo hiyo sehemu yake. Wabunge indelee kama kawaida wachaguliwe na watu wa constituency yake lakini mambo ya kusema wakikosa, watolewe kabla ya uchaguzi kwa vote of no confidence, ningetilia mkazo hapo wangoje miaka mitano. Kwa sababu huwezi kuwa ulichaguliwa na 100% kwa hivyo kuna wale hata kama ni 2%

wataanza kulalamika na itakuwa tunafanya hiyo kazi ya uchaguzi kila wakati.

Haki kwa watoto wa kike nitazungumzia hapo, ama mwanamke kwa jumla, wanawake wapewe haki kila mahali kama ni Bungeni tukisema one third ndio tunataka wawe wamechaguliwa, na kama hawajachaguliwa tunasema wale nominated at least tuweke kiwango fulani kwamba ndio watakuweco. Hata kama tukisema 12 ndio watakuwa nominated tukisema ni wote bora wawe wanawakilisha jambo fulani kama ni disabled, tunaweka mwanamke na awe disabled ili waweze kufikisha ile a third of the MPs.

Ile ingine kwa County Council ningependa iwe pia hivyo, kwamba tukisema ni one third, wawe one third na kama hawatoshi tunahakikisha kama wale nominated, wawe nominated ili wajaze ile nafasi.

Haki ya mtoto msichana hasa katika hawa watu wa kuhama hama ningependa ya kwamba kulazimishwa kuolewa hiyo iondolewa kabisa hasa wakati huu ambao kuna janga la ukimwi, utalazimishwa na mtu ana ukimwi, bibi amekufa na hawaja-confirm ni nini imemua, unalazimishwa na inakuwa shida kwako na kwa familia. Kwa hivyo ndoa ya lazima mimi nasema hiyo itolewe kabisa, mtu aolewe kwa hiari, kwa mtu ambaye amependa.

Kwa elimu, huwa tunaposa watoto wadogo sana hiyo pia ningependa iwe ni sheria na sheria itiliwe maanani maana sasa inasema msichana akiwa na miaka kumi na tano ati ana haki ya kuamua kuolewa na tuna hakika kwamba msichana wa miaka kumi na tano hawezi kuwa amemaliza shule. Kwa hivyo mimi ningeweka kiwango niseme ni ishirini na tano na huyo mtoto atakuwa amesoma mpaka University ama mwisho ambao atakuwa amefika. Hiyo pia ningependa iwe sheria hata kwa kuolewa kwa hiari kwa sababu siku hizi watoto wa miaka tisa anasema anataka kuolewa. Kwa hivyo hiyo mimi ningesisitiza kabisa kwamba iwe ni sheria, mtoto wa miaka tisa au kumi na mbili hawezi kuolewa. Nafikiri nimemaliza.

Com. Lethome: Thank you Margaret. Joseph Kariuki.

Joseph Kariuki: Basi mimi nitasoma utangulizi.

Com. Lethome: Anza kwa jina lako.

Joseph Kariuki: Jina langu ni Joseph Kariuki Karunga. Basi mimi nitaeleza vile naona inafaa na kwanza nitaanza tu kama kwa hii Katiba yetu ya mbeleni kuna ile zitageuka na kama kuna ile inafaa itaendele. Nikianza na hiyo yetu ya mbeleni kuanzia tu kuna utangulizi, utangulizi wetu wa Kenya iwe umoja, upendano wa wananchi, taifa moja.

Ukubwa upewe Rais na Bunge.

Uraia, mwananchi kamili ni raia wa Kenya, wasichana nao wapewe uraia, yoyote aliyezaliwa Kenya alinde Kenya. Raia wa Kenya waiendeleze wenyewe.

Ulinzi na usalama wa taifa upewe Rais na Bunge na serikali.

Vyama vya kisiasa viandikishwe kwa serikali na visimamiwe na serikali.

Muundo na aina ya serikali, Rais, Bunge na Waziri Mkuu aliyeteuliwa na Rais na Bunge. Waziri anaweza kuwa na wasaidizi wake, hata Rais anaweza kuwa na msaidizi wake na hata Bunge pia.

Bunge: Bunge itunge sheria na Rais akubali na kuona ni sawa kwa wananchi. Kama Mbunge amedanganya wananchi wake atolewe wakati wowote Wabunge wasitutegemee, yaani Wabunge na ma-Councillors kama wanatudanganya kwa kutufanyia maendeleo na wasifanye basi inafaa kuwatoa hata kama muda hujaiisha, pia walipwe na serikali. Kwa wale tuliochaguwa, elimu iwe mbele na mamlaka ya nchi iwe kwa Rais kwa kipindi cha uongozi. Bunge laweza toa Rais na Rais naye pia anaweza kutoa makosa kwa Mbunge, yeye pia anaweza kutoa Mbunge. Utawala wa mkoa utoke wa Rais.

Maofisa wa mahakama wahakikishe haki inafuatwa. Mahakimu wawe wasomi sana kimaendeleo na elimu. Ma-judge wawe ni watu ambao wako na elimu.

